# Nipashe

Jumamosi Machi 30, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579879

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Serikali sasa kupanga bei elekezi dawa za binadamu

UKURASA 5




UKURASA 13

# Kigogo Takukuru aburuzwa kortini

UKURASA 2



Aliyekuwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzui ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kulthum Ahmed Mansoor, akiwa chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa mashtaka ya uhujumu uchumi yakiwamo manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha zaidi ya shilingi bilioni 1.4. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

### ASKARI MBARONI KWA TUHUMA ZA MAUAJI

ASKARI wanne wa Jeshi la Magereza mkoani Morogoro, wanashikiliwa na polisi kwa madai ya...

**UKURASA WA 3**

### TANZANIA YAPATA MASHINE ZA KISASA KUTIBU SARATANI

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amezindua mashine za kisasa za tiba ya saratani katika...

**UKURASA WA 3**

### ALIVYOOKOLEWA NDOA UTOTONI NDANI YA SHELA

MWANAFUNZI katika shule moja Tinde wilayani Shinyanga, amesimulia alivyookolewa katika ndoa...


## Diwani wa CCM achongea wabunge

UKURASA 9



## Joshua Nassari akwaa kisiki mahakamani

UKURASA 2


MICHEZO **YANGA YAIPANIA ALLIANCE FA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Askari Magereza mbaroni tuhuma mauaji ya mfugaji

**Na Idda Mushi,** MVOMERO

ASKARI wanne wa Jeshi la Magereza mkoani Morogoro, wanashikiliwa na polisi kwa madai ya kumuua mfugaji wa jamii ya Kimasai, Lepeti Mandero (20), mkazi wa kijiji cha Mtakuja, Dakawa wilayani Mvomero. Mandero anadaiwa kuuawa na askari hao wa Gereza la Mbigiri baada ya kupigwa risasi ya kiunoni.

Imedaiwa kuwa Lepeti alipigwa risasi baada ya yeye na wenzake kuingiza na kulisha mifugo kwenye pori linalomilikiwa na jeshi hilo, huku ng'ombe watano wakidaiwa kufa katika tukio hilo na wengine zaidi ya 100 wakishikiliwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, amethibitisha kuuawa kwa kijana huyo Machi 27, mwaka huu, majira ya saa tatu asubuhi katika mashamba pori hayo ya Magereza Mbigiri na tayari wamefungua jalada la uchunguzi. Aliwataja askari Magereza wanaoshikiliwa ni Sajenti Roma, Koplo Barnabas, Wada Albart na Wada Tatius ambao wote ni askari wa Gereza la Mbigiri lililoko wilayani Kilosa.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda Mutafungwa alisema askari hao walikuwa kwenye operesheni ya kuondoa mifugo ndani ya shamba la miwa la Magereza, lakini ghalfa walimwona kijana huyo akiwa na makundi mawili ya ng'ombe na walipojaribu kuzuia ng'ombe hao, kijana huyo aliyekuwa na wenzake, walianza kuwashambulia askari kwa sime, rungu na fimbo.

Kamanda alisema katika mapambano hayo, askari Magereza walianza kufyatua risasi hewani ili kuwatawanya vijana hao, lakini kijana huyo na wenzake waliendelea kuwashambulia ndipo askari mmoja alipofyatua risasi na kumjeruhi kiunoni karibu na tumbo na kusababisha kifo chake. Alisema tayari mwili wa marehemu umeshafanyiwa uchunguzi wa kitabibu na ndugu wameshauchukua kwa ajili ya maziko.

Hata hivyo, kamanda Mutafungwa alitoa wito kwa wananchi kutoingia na kufanya shughuli za kilimo, ufugaji na nyinginezo za kibinadamu kwenye maeneo ya serikali, majeshi na hifadhi.

Juzi, timu ya waandishi wa habari, baada ya kupata taarifa za mauaji hayo, ilikwenda nyumbani kwa familia ya marehemu katika kijiji cha Mtakuja, Kata ya Doma na kukuta jamii ya wafugaji wakiwa wamekutana kujadili tukio hilo.

Mmoja wa vijana waliokuwa wameambatana na Mandero katika tukio hilo, Sumai Sadru, alisema walikwenda katika mashamba hayo eneo ambalo halikuwa na mazao isipokuwa mapori na majani na kuanza kulisha mifugo, lakini ghafla walitokea askari Magereza wawili wakiwa na sare na silaha.

Alisema kwa hofu waliyokuwa nayo walianza na wao kuswaga mifugo kuiondoa shambani humo, lakini askari wale walianza kurusha risasi chini na kuwaua ng'ombe watano na kumjeruhi mwenzao mmoja kiunoni ambaye risasi ilipenya upande mmoja na kutokea upande mwingine. "Tulivyoona wameondoka tulirudi nyuma na kumwangalia mwenzetu akiwa anavuja damu nyingi na alifariki dunia," alisema kijana huyo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika (kushoto), akimsikiliza mjane wa Baba wa Taifa, Mama Maria Nyerere, alipomtembelea nyumbani kwake jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake. Kulia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa. **PICHA: UTUMISHI**

# Mkurugenzi Takukuru kortini tuhuma za utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor (57), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumu yakiwamo manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477.

Mansoor alisomewa mashtaka jana saa 5:46 asubuhi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Wankyo Simon, alidai kuwa kati ya Januari 2013 na Mei, mwaka jana katika ofisi za Takukuru, Upanga jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alighushi barua ya toleo la ardhi ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, huku akijua kuwa si kweli.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa kati ya Januari, 2012 na Mei, 2017 eneo la Upanga, Ilala jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini Takukuru, kwa njia ya udanganyifu alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alijipatia fedha hizo baada ya kudanganya kwamba angemuuzia kiwanja katika kijiji cha Ukuni, Bagamoyo mkoani Pwani. Shtaka la tatu, la nne, la tano, la sita na la saba, ilidaiwa kuwa tarehe na mahali pa tukio la pili, mshtakiwa alijipatia kwa njia ya udanganyifu Sh. milioni 27 kutoka kwa watu watano tofauti.

Wankyo alidai kuwa mshtakiwa alijipatia fedha kutoka kwa Wakati Katondo, (Sh. milioni tatu), Gogo James (milioni tano), Ekwabi Majungu (milioni saba), John Amos (milioni saba) na Rose Anatory Sh. milioni tano, ambao wote hao wanadaiwa kuwa ni watumishi wa Takukuru.

Katika shtaka la nane, ilidaiwa kuwa kati ya Januari, 2013 na Mei, mwaka jana, eneo la Upanga, mshtakiwa alitakatisha Sh. 1,477,243,000 wakati akijua kuwa fedha hizo ni zao la kosa tangulizi la kughushi.

Hata hivyo, kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote. Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 12, mwaka huu.

# Nassari akwaa kisiki mahakamani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma, imetupilia mbali ombi la aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki (Chadema), Joshua Nassari, la kufungua kesi ya msingi ya kutengua uamuzi wa Spika Job Ndugai wa kumvua ubunge.

Ombi hilo limetupwa kutokana na maelezo kuwa haukuwa uamuzi wa Spika bali ni matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Latifa Mansour, baada ya kusikiliza maombi ya mbunge huyo na majibu ya upande wa Jamhuri.

Jaji Mansour alisema ombi hilo limetupiliwa mbali kutokana na uamuzi ulitolewa kuwa si wa Spika Ndugai binafsi, bali wa kanuni za kudumu za bunge kama inavyoelekezwa.

"Kanuni za Kudumu za Bunge zinaelekeza kuwa mbunge anakoma kuwa mbunge kutokana na kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo, hivyo basi uamuzi uliotolewa na bunge si wa Spika bali ni kanuni hizo ndizo zilizomwondoa katika nafasi ya ubunge Nassari," alisema Jaji Mansour.

Aliongeza kuwa kutokana na hali hiyo, mbunge kama aliona hajatendewa haki alipaswa kuandika barua ya malalamiko kwenda kwa Katibu wa Bunge na si mahakamani.

Aidha, Jaji Mansoor alisema kutokana na hukumu hiyo, kama kuna mtu atakuwa hajaridhika na uamuzi wa mahakama anaruhusiwa kukata rufani.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya Mahakama, Wakili wa Nassari, Fred Kalonga, alisema wanaupokea uamuzi wa mahakama lakini watakwenda katika ngazi nyingine zaidi ili mteja wake apate haki.

"Hatuishii hapa, lazima tukate rufani katika mahakama ya rufani ili kupata tafsiri zaidi ya hiki ambacho tulikileta mahakani hapa. Jaji ametuambia kuwa Nassari alitakiwa kuandika barua ya malalamiko kwa katibu wa mbunge, lakini kimsingi kwa kauli ya Spika Ndugai, huyu si mbunge tena kwa sababu tayari jimbo lilishatangazwa kuwa wazi. Kwa mantiki hiyo, tusingeweza kuandika barua kwa kuwa yule si katibu wake tena," alisema Kalonga.

Naye Nassari alisema ili dhahabu ing'ae ni lazima ipitie katika moto mkali, hivyo wananchi wake wa Arumeru Mashariki wanatakiwa kutokuwa na hofu yoyote kwa kuwa yatakwisha.

"Mimi katika ubunge wangu nimepitia mambo makubwa sana ikiwamo kuanguka na ndege, lakini hakuna aliyekufa hata mmoja kwenye ile ajali. Pia nilishavamiwa nyumbani na watu wakiwa na silaha za moto lakini waliishia kuua mbwa tu, hivyo haya kwangu ni madogo na kwa sababu tuko na Mungu natumaini yatapita," alisema.

Machi 20, mwaka huu, Nassari aliwasilisha ombi mahakamani hapo kufungua kesi ya msingi dhidi ya Spika baada ya kumvua ubunge.

INAENDELEA UK. 8

## HABARI ZA KITAIFA

# Upelelezi kesi vigogo Barrick ngoma nzito

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayomkabili aliyekuwa Rais wa Migodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu, Deogratius Mwanyika na wenzake, umedai mahakamani bado unaendelea na upelelezi chini ya usaidizi wa nje ya nchi.

Mwanyika na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 39, ikiwamo kutakatisha fedha na kukwepa kodi zaidi ya Dola za Marekani milioni 112.

Madai hayo yalitolewa jana na Wakili wa Serikali, Simon Wankyo, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Kevini Mhina.

"Mheshimiwa Hakimu upelelezi wa kesi hii bado unaendelea chini ya usaidizi wa nje ya nchi. Tunaomba tarehe nyingine ya kutajwa," alidai Wankyo.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 12, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Mwanyika, washtakiwa wengine ni Meneja Uhusiano wa Mgodi wa Bulyanhulu, Alex Lugendo; Mkurugenzi Mtendaji wa Pangea, North Mara na Bulyanhuku, Assa Mwaipopo, kampuni ya Mgodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Oktoba 17, mwaka jana.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matatu ya kula njama, mashtaka saba ya kughushi, mashtaka 17 ya utakatishaji wa fedha, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) shtaka moja, kuongoza uhalifu wa kupangwa shtaka moja, mashtaka manane ya kukwepa kodi na moja la kutoa rushwa.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Aprili

INAENDELEA UK. 8



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo juu ya mashine ya kisasa ya tiba ya saratani kwa mionzi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Maiselage, baada ya kuzindua jengo na mashine za tiba ya saratani, katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# Tanzania yapata mashine za kisasa kutibu saratani

**Na Mary Geofrey**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amezindua mashine za kisasa za tiba ya saratani katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), ambazo ni za kwanza kuwapo katika nchi za Afrika.

Mashine hizo zinazotambulika kwa jina la CT Simulator na mashine mbili za tiba ya mionzi kwa teknolojia ya kisasa aina ya Linear Accelerator, zimenunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni 9.5 na zitaokoa Sh. bilioni 7.5 zilizokuwa zinaigharimu serikali kila mwaka kwa wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

Akizindua mashine hizo jana jijini Dar es Salaam, Samia alisema zitasadia kuingizia mapato hospitali hiyo na kupunguza utegemezi wa fedha za serikali.

"Kuwapo kwa mashine hizi za kisasa nchini ambazo hazipo Afrika nzima, zitawezesha wagonjwa wa sekta binafsi kufuata huduma hii na wanaotoka nje ya nchi kuja nchini kufuata matibabu na hivyo itaiwezesha Ocean Road kupata fedha zitakazosaidia taasisi kujiendesha na kununua mashine nyingine kama hizi," alisema Samia.

Makamu wa Rais aliusihi uongozi wa taasisi hiyo kuitangaza huduma hiyo nchi nyingine ili wagonjwa waliokuwa wanapelekwa India na nchi nyingine duniani waletwe nchini kupata matibabu.

"Wagonjwa wa nchi zingine waletwe kupata matibabu ya kulipia na si bure. Kama sera ya nchi yetu inavyosema matibabu

INAENDELEA UK. 8






# Asimulia alivyookolewa ndoa utotoni akiwa ndani ya shela

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI katika shule moja Tinde wilayani Shinyanga, amesimulia alivyookolewa katika ndoa ya utotoni akiwa ndani ya shela, kwa kutolewa mahari ya ng'ombe 19 na kukatishwa masomo ya sekondari alipokuwa kidato cha kwanza.

Mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa) alisema tukio hilo lilitokea mwaka 2016 akiwa na miaka 14, wakati huo akiwa amefaulu na kuchaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari, lakini baba yake aligoma kumsomesha na kuamua kumtafutia mume wa kumuoa.

Alisema siku ya harusi, akiwa ndani ya shela, Shirika la Agape kwa kushirikiana na polisi wakatibua ndoa hiyo.

Mwanafunzi huyo ambaye kwa sasa anasoma kidato cha pili kupitia mfumo wa elimu ya watu wazima katika shule moja ya sekondari mjini hapa, alitoa simulizi hiyo juzi, wakati baadhi ya madiwani wa halmashauri kutoka mikoa mitano, wakiwa na viongozi wa vituo vya taarifa na maarifa kutoka mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), walipotembelea shule hiyo ya waathirika wa mimba na ndoa za utotoni.

"Nalipongeza sana Shirika la Agape na Jeshi la Polisi kwa kuokoa ndoto yangu isizimwe. Baba yangu alikuwa hapendi kabisa kunisomesha na kuamua kunitafutia mwanamume ambaye hata simjui. Nilikuja kumwona siku hiyo hiyo ya harusi akitokea Tabora kwa tamaa zake za kutaka mifugo," alisema.

INAENDELEA UK. 8

# Ofisa usalama ashtakiwa kesi ya uhujumu uchumi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

OFISA Usalama wa Wilaya ya Ngorongoro mkoani hapa, Issa Ng'itu (54), na Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwindaji ya Otterlo Bussiness Corporation (OBC) Ltd, Isaya Mollel, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha na kusomewa mashtaka (15), yakiwamo uhujumu uchumi na kughushi nyaraka kwa ajili ya kujipatia mali kinyume cha sheria.

Aidha, Mollel alitolewa mahabusu katika Gereza la Kisongo na gari lenye namba za usajili STK 5720 na anakabiliwa na kesi nyingine ya uhujumu uchumi.

Akisoma mashtaka hayo jana mbele ya Hakimu Mfawidhi Obadia Bwegoge, Wakili Mkuu wa Serikali Oswald Tibabyakoma, akisaidiwa na Mwanasheria Mwandamizi wa Serikali Mkoa wa Arusha, Materinus Marandu, alidai kuwa kati ya mashtaka 15,

INAENDELEA UK. 8



Mama akiruka matope katika eneo la Msasani sokoni, kutokana na mvua zilizoanza kunyesha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanafunzi aporwa baiskeli kisha kunyongwa hadi kufa

**Na Steve Chindiye,** TUNDURU

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Muhuwesi, Tariq Mohamed (16), amefariki dunia katika tukio la kutatanisha na kuporwa baiskeli na karanga ambazo alikwenda kuzichukua shambani baada ya kutumwa na wazazi wake.

Tukio hilo lilitokea juzi baada ya mwanafunzi huyo kutorejea nyumbani kutoka shambani kufuata karanga ambazo zilipangwa kwa matumizi ya kuungia mboga.

Imeelezwa kuwa watu waliofanya unyama huo, kabla ya kumuua, walimfunga kitambaa usoni na kamba mikono yake kwa nyuma.

Baba mzazi wa kijana huyo, Issa Mohamed, alisema mtoto huyo alitumwa na mama yake mzazi, Sofia Said, kwenda kufuata karanga hizo shambani baada ya kurudi kutoka shuleni.

Inadaiwa kuwa siku hiyo kulikuwa na mitihani ya majaribio kwa wanafunzi wa darasa la saba, hivyo wanafunzi wengine hawakutakiwa kuwapo shuleni ili kuwezesha kuleta utulivu.

Alisema baada ya kupokea taarifa za kutorejea kwa kijana wake, aliambatana na watu watatu kwa ajili ya kwenda kumtafuta bila mafanikio na kwamba baada ya hapo, alitoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya kijiji na kata na baadaye kituo cha polisi kwa ajili ya msaada zaidi.

Mohamed alisema siku ya pili, wananachi wakisaidiana na viongozi wa serikali ya kijiji na kata, walifanya msako katika eneo la njia ya kuelekea mashamba yaliyoko katika eneo la Chasa na kuukuta mwili wa kijana huyo ukiwa umetelekezwa katika vichaka.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa Tariq, Dk. Alfred Mabena, alisema kifo hicho kilisababishwa na tukio la kunyongwa na kuvunjwa mifupa ya shingo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, amedhibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba polisi wanamshikilia Noel Nasoro kwa ajili ya uchunguzi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 29/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **02/04/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR** kuelekea **KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili: **T785 CAD/T 166 ADN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21.80 |
| Upana | - | mita | 3.40 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

3. NJia itakayotumika **DAR** hadi **KAGERA** kupitia **MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215148402


# Mvua ya mawe yaharibu mazao

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

MVUA kubwa ya mawe iliyoambatana na upepo mkali iliyonyesha kwa muda wa takribani dakika 35 katika Kijiji cha Makilawa, Ikungi mkoani Singida, imeharibu zaidi ya ekari 400 za mazao mbalimbali yakiwamo mahindi.

Mtaalamu wa Kilimo na Mifugo wa Kata ya Makilawa, Bode Kiimu, alisema jana kuwa mvua hiyo iliyoanza kunyesha majira ya jioni ikiwa na upepo mkali na mawe, imewasababishia wananchi wa kijiji hicho hasara ya Sh. 33,300,000 kutokana na kuharibika kwa mazao ya chakula na biashara.

Mbali na mahindi, mtaalamu huyo aliyataja mazao na ekari zilizoharibiwa na mvua hizo kuwa ni pamoja na ekari 283 za mahindi, ekari 111 za alizeti, mtama ekari 11, ekari tano za pamba na viazi vitamu ekari 1.5.

Kwa mujibu wa Kiimu, kutokana na athari hiyo kuna uwezekano wa kaya 25 zenye jumla ya wakazi 250 kukumbwa na baa la njaa mwaka ujao. "Mvua ilianza kunyesha muda wa saa 12:00 jioni ikiwa na upepo mkali na baada ya upepo mkali kupita, upepo ulisimama na ndipo yakaanza kuteremka mabarafu ambayo yamekaa kwa muda wa siku nne ndipo yakayeyuka na kuharibu mazao mbalimbali," alisema.

Wakulima wa kijiji hicho, walisema walikuwa na ndoto kubwa ya kuvuna mazao mengi ya chakula na biashara, lakini sasa wamejikuta ndoto hiyo ikitoweka kutokana na mvua hiyo kubwa ya mawe.

Kwa upande wake, Diwani wa Makilawa, Shaaban Mtakii, alisema baada ya tukio hilo kutokea, uongozi wa kata ulichukua hatua za kutoa taarifa ngazi ya wilaya ambako ofisa maendeleo ya kilimo alijulishwa kwa barua, lakini hawajafika kwenye tukio hilo.

"Baada ya tukio hilo kutokea, ofisa kilimo na mifugo wa kata ya Makilawa, alitembelea mashamba na kufanya tathmini kisha kuujulisha uongozi wa wilaya, lakini mpaka sasa bado hawajafika kwenye tukio hili na sielewi ni kwa sababu gani, ila habari wanazo," alisema.

Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Makilawa, Nkungu Njokha, aliweka bayana kuwa tukio hilo lilitokea juzi, baada ya wingu kujikusanya kwenye eneo hilo lenye kaya 25 na mvua kuanza kunyesha kubwa, huku mawe yakishuka chini.

HABARI KITAIFA

# Serikali kupanga bei elekezi dawa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema inatarajia kupanga bei elekezi ya dawa za aina zote ili kuleta ushindani wa haki wa huduma hiyo kwenye soko.

Msajili wa Baraza la Famasi, Elizabeth Shekalaghe, alisema hayo juzi, wakati wa semina ya uhamasishaji wa wahariri na waandishi wa habari na uzinduzi wa jarida la baraza hilo.

Akizungumza kwenye semina hiyo, Shekalaghe alitolea mfano kwamba nje ya Hospitali ya Temeke kumejaa maduka ya dawa ambayo mgonjwa akitoka hospitalini anadakwa kama nzi.

"Unakuta maduka yameongozana eneo moja. Mtu akitoka tu Hospitali ya Temeke anaambiwa njoo huku, njoo huku. Hii inaathiri sana ubora wa huduma kwa sababu itafika mahali mtu mwingine atashindwa biashara. Kikubwa tunachokifikiri ndani ya Wizara ya Afya (Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto), ni kupanga bei elekezi ya dawa," alisema.

Shekalaghe alisema wakishapanga bei matatizo yote yatakwisha.

"Tunataka ukinunua dawa Kinondoni, ukinunua Ilala bei ya dawa fulani iwe inajulikana, hivyo hakutakuwa na ushindani bali utoaji huduma," alisema.

Alisema tatizo lililopo kwenye utoaji wa huduma kwenye maduka hayo ni wahusika kuchukulia kuwa uuzaji wa dawa ni biashara badala ya huduma.

Akizungumzia umbali wa duka moja hadi lingine, Shekalaghe alisema kwa mujibu wa utaratibu ilikuwa ni mita 300, lakini baada ya wahusika kulia walipunguza hadi kufikia mita 150.

"Umbali huu unahusu maduka ya rejareja ila ya jumla hakuna umbali uliowekwa kwa sababu wao wanauza dawa kwa kampuni fulani, tuliposema mita 300 kwa maduka ya rejareja wananchi wakalia tukapunguza kufika mita 150, lakini bado wanalia kwa sababu kila mtu anataka huduma iwe karibu," alisema.

Alisema wanaamini kwamba mpango wa kufuata utaratibu wa umbali wa duka moja la dawa la rejareja na lingine utafanikiwa jijini Dodoma ambako mipango miji ndiyo inafanyika.

Alisema changamoto iliyopo ni kwamba mtu akiona jengo anataka kuweka duka la dawa na anapoambiwa kwamba kwa mujibu wa taratibu umbali unaotakiwa kati ya duka na duka ni mita 150 anaona anaonewa.

Shekalaghe alisema mwarobaini wa uuzaji dawa bila vyeti kwenye maduka ya dawa utatatuliwa hivi karibuni kupitia kanuni mpya kwa kuwa lengo ni kudhibiti utoaji wa huduma hizo kinyume na taratibu.

"Mteja akienda duka la dawa na ukimtilia shaka muuzaji una haki ya kumuomba akuonyeshe cheti chake kwa sababu wengine wapo tu, lakini hawana sifa na hawajui matumizi ya dawa wanaouza," alisema.

"Tuna kesi tisa za aina hiyo ambazo tunaamini zitaleta matokeo mazuri zikiisha na hawa watoa huduma wababaishaji watakuwa fundisho kwa wengine," alisema.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Oterlo Business Corporation Ltd (OBC), Isaya Mollel, akiingizwa mahabusu ndogo, katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha jana, baada ya kusomewa mashtaka 15, likiwamo la uhujumu uchumi na kughushi nyaraka za serikali. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Kasi usambazaji umeme yamkera Naibu Waziri

**Na Steven William,** MUHEZA

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, ameonyesha kutoridhishwa na usambazaji wa umeme vijijini katika Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Kutokana na hatua hiyo, ameamwagiza mkandarasi, Kampuni ya Radi inayotekeleza mradi huo uliosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) awamu ya tatu, kuongeza vituo vya kufanyia kazi kutoka kimoja kilichoko sasa hadi vitano, ili kuongeza kasi ya usambazaji wa nishati hiyo.

Mgalu alisema hayo jana, wakati akizungumza na mkandarasi huyo katika ziara yake ya siku moja iliyoambatana na uzinduzi wa umeme katika vijiji vya Mamboleo na Lusanga.

Alisema anataka kuhakikisha wananchi wanapata umeme kwa haraka katika Wilaya ya Muheza kwa kuwa hiyo ni haki yao.

Mgalu alisema anawashangaa makandarasi wanakuwa na kituo kimoja cha kufanyia kazi jambo ambalo si zuri, hivyo waongeze haraka sana ili mambo yaende haraka.

Naibu Waziri huyo alisema hayo baada ya Mbunge wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu, kumweleza kuwa katika wilaya ya Muheza wamepata vijiji 19 katika mradi wa REA awamu ya tatu, lakini mpaka sasa umeme umewaka katika vijiji vitano tu.

Katika hatua nyingine, naibu waziri aliwaeleza wananchi wa Wilaya ya Muheza kwamba bei ya kulipia umeme ni Sh. 27,000 na si vinginevyo.

# EAC waja na mwarobaini udanganyifu mitihani

**Na Beatrice Shayo**

KUANZISHWA kwa Umoja wa nchi za Afrika Mashariki katika Tathmini ya Elimu (EAAEA), kutasaidia kutatua changamoto ya udanganyifu na wizi wa mitihani, imeelezwa.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani (Necta), Dk. Charles Msonde, ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa umoja huo ambao umeanzishwa na mabaraza na bodi za mitihani za nchi za Afrika Mashariki alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam.

Alisema miongoni mwa sababu za kuanzishwa kwa EAAEA ni kubadilishana uzoefu katika kudhibiti udanganyifu na mianya inayotumika katika ukiukwaji wa uendeshaji mitihani ya taifa.

"Huu umoja utatusaidi kupambana na changamoto ya udanganyifu na wizi wa mitihani inayotokea katika mataifa yetu.

Umoja siku zote ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kuwapo kwa watu wote hao itatuwezesha kuwa na mawasiliano ya pamoja katika kuhakikisha tathmini inakuwa bora na haina udanganyifu wala wizi ya mitihani."

Alisema kuanzishwa kwa umoja huo kunalenga mambo mbalimbali ikiwamo ujuzi na uelewa na kwa watendaji wa mabaraza ya mitihani, kuwezesha uzoefu ili kuimarisha tathmini ya elimu bora katika nchi za Afrika Mashariki na kutoa fursa ya kujipanua ujuzi na maarifa katika suala nzima la tathmini.

Kwa mujibu wa Msonde, umoja huo utasaidia kutoa mchangao wa kitaalamu kwa viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika tathmini ya elimu.

Dk. Msonde alisema wazo la kuanzishwa kwa umoja huo lilitolewa Machi mwaka jana, katika mkutano wa wakuu wa mabaraza na bodi za mitihani za nchi husika.

"Wataalamu kutoka nchi hizo waliunda timu na kupewa jukumu la kuandaa rasimu ya katiba ambayo inatumika katika uendeshwaji wa umoja, hivyo wakuu wa mabaraza na bodi za mitihani wameidhinisha katiba hiyo ili kuhakikisha upimaji wa tathmini inaboreshwa na ushirikiano unakuwa imara," alisema.

Dk. Msonde alisema wamekutana nchi nne kwa ajili ya kupitia katiba na kuidhinisha ili iweze kufanya kazi mara moja kwa ajili ya kuendesha shughuli za tathmini na upimaji elimu ulio bora katika mataifa ya nchi za Afrika Mashariki.

Naye Katibu Mkuu wa EAAEA, Dan Odongo, alisema umoja huo unatumiwa na wataalamu wa tathmini, wakuza mitaala, wataalamu na watafiti kubadilishana utaalamu na uzoefu katika kanda zao.

Alisema watakwenda kubadilishana uzoefu katika tathmini ya elimu katika nchi za Afrika Mashariki.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Rais Magufuli kuibeba Serengeti Boys

**TIMU** ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Boys itakuwa mwenyeji wa Fainali za Afrika kwa umri huo zitakazofanyika hapa nchini kwa mara ya kwanza.

Fainali hizo zinazosimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) zinatarajiwa kuchezwa kuanzia Aprili 14 hadi 28 mwaka huu.

Hii ni mara ya pili kwa Serengeti Boys kushiriki fainali hizo, mara ya kwanza ilikuwa mwaka juzi huko nchini Gabon.

Kwa sasa kikosi hicho cha Serengeti Boys kiko jijini Kigali kikishiriki mashindano maalumu ambayo yanajumuisha timu za nchi tatu ambazo ni pamoja na wenyeji Rwanda na Cameroon.

Katika kuhakikisha kuwa Serengeti Boys inaingia katika mashindano hayo ikiwa imara, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli, ametangaza kuwapatia kiasi cha Sh. bilioni moja.

Kiasi hicho cha fedha kilichotolewa na Rais Magufuli, ni maalumu kwa ajili ya kukiandaa kikosi cha timu hiyo ili kiweze kufanya vema katika fainali hizo.

Rais Magufuli anataka kuona wenyeji wanakuwa imara na kupata matokeo mazuri katika mechi zote watakazocheza kwenye fainali hizo na si kuwa wasindikizaji.

Huo ni mwanzo, timu hiyo ambayo inahitaji kuweka kambi Ulaya, vifaa vya michezo na posho za wachezaji pamoja na viongozi, inahitaji fedha zaidi ili iweze kutimiza malengo yake.

Inafahamika wazi kuwa mbali ya heshima ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo, timu nne zitakazofanya vema zitakuwa zimekata tiketi ya kushiriki katika Fainali za Dunia za Vijana zijazo ambazo zitafanyika Peru.

Katika mpira hakuna miujiza, timu itakayojiandaa vema, wachezaji watakaojituma na watakaoshinda mechi zao, ndio wana nafasi kubwa ya kutimiza malengo ya kucheza fainali hizo za dunia.

Rais Magufuli ameanzisha safari, huu ni wakati kwa kampuni, taasisi na wadau wengine wa ndani na nje ya Tanzania kujitokeza kuichangia Serengeti Boys ili iweze kutimiza ndoto zake.

Kwa pamoja hakuna kisichowezekana, Serengeti Boys inahitaji mchango wa kila Mtanzania ili iweze kutekeleza malengo yake na kikubwa ni kuitangaza nchi.

Nipashe inaamini kuwa, kufanya vema kwa Serengeti Boys ndio kutasaidia kulitangaza jina la Tanzania katika medani mbalimbali za kimataifa na kutaongeza pato la uchumi kwa wageni watakaokuja nchini.


Huu ndio wakati sahihi wa kushiriki katika kuiimarisha timu hiyo na si kusubiri baadaye kuanza kuikosoa au kuiponda endapo itapata matokeo yasiyofurahisha.

Kama nguvu ziliweza kuunganishwa na hatimaye Timu ya Taifa (Taifa Stars) kufanikiwa kukata tiketi ya kucheza Fainali za Afrika zitakazofanyika Juni, mwaka huu (AFCON 2019), pia inawezekana kuhakikisha ndoto za Tanzania zinatimia kwa kucheza Fainali za Dunia za Vijana kwa mara ya kwanza.

Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, Watanzania huu ni wakati wa kujitoa kuhakikisha timu zetu zote za Taifa ikiwamo ye wanawake (Twiga Stars) zinafanya vema katika mashindano mbalimbali ambayo zitashiriki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Lililopo ndilo lisemwalo

**JAMBO** linalosemwa au linaloongelewa juu yake ni lililopo. Lisilokuwapo halisemwi. Hutumiliwa mtu anayelikana jambo fulani kisha akawa hataki kukubali ingawa watu wengine wanaufahamu ukweli wake.

Nimeandika mara nyingi kuhusu ukata (ufukara; ukochele, umasikini) wa klabu ya Yanga kuwa unasababishwa na baadhi ya viongozi wanaotumia fedha kuwaghilibu baadhi ya wanachama hohehahe kuwashawishi wenzao ili wachaguliwe!

"Wajinga ndio waliwao" maana yake wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii yaweza kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana.

Viongozi walaghai wanapaswa kusoma methali hii: "Wajua tamu ya ua, sumu wanipiani?" Maana yake unajua ua ndilo lenye utamu, kwa nini wanipa sumu? Huweza kutumiwa kwa mtu anayemfanyia mwenzake/wenzake jambo baya ingawa analifahamu lililo zuri.

Kama viongozi wa aina hiyo wanataka kuisaidia klabu, sioni sababu ya kupita matawini na kuwahonga baadhi ya wanachama wenye njaa ili wapigiwe debe kuwa eti ndiwo wanaofaa! Haiingii akilini kwamba mtu anayetaka kutoa msaada huweka baadhi ya watu wamsaidie kuwashawishi wanachama ili achaguliwe!

Mmoja wa viongozi alitangaza kujiuzulu, alisema ni vigumu kuishi katika familia ambayo baba anakula vizuri na kulala pazuri, lakini watoto wake wanapita kwa majirani kuomba msaada bila kujua kesho yao itakuwaje.

Ndivyo ilivyo sasa pale Yanga huku kocha wao, Mwinyi Zahera akifanya kila liwezekanalo kuwatuliza wachezaji licha ya kupigwa vita vya chini chini na haohao wanaoifisidi klabu!

Anasisitiza kuwa katika klabu ya Yanga mambo ni magumu kwa kuwa baadhi ya viongozi wasiokuwa na huruma na wachezaji wanaolipwa mishahara kwa shida! Anasema katika kipindi chake cha uongozi aliwashauri wenzake jinsi viongozi bora wanavyotakiwa kuwa lakini walim-beza na kumtenga!

Kuna kauli aliyotoa inayomfanya kutoeleweka. Kwamba "kupiga haikatazwi, lakini ifike sehemu tuone huruma na hawa watoto (wachezaji)."

Ameamua ajitoe katika dhambi hiyo kubwa ili yasimkute makubwa. Kwa lugha ya mitaani, 'kupiga hela' maana yake ni kula hela zisizokuhusu; matumizi au kujinufaisha kwa fedha za udokozi (tabia ya mtu kuiba vitu/fedha kidogo kidogo).

Hapa ndipo penye kirumbizi/kiumbizi (ngoma inayochezwa na watu wawili wawili kwa kupigana kwa fimbo). Hebu turejee tena maneno aliyosema kuwa "kupiga haikatazwi." Maana yake ni kwamba anakiri kuwa kudokoa fedha za klabu haikatazwi ila wadokozi wawe na huruma kwa wachezaji.

Udokozi ni wizi. Usiibe: Amri ya saba ya Mungu yakataza kuchukua na kuwa na mali ya jirani bila haki na kumtendea ubaya kwa namna yoyote kuhusu mali yake. Inaamuru haki na mapendo katika kutunza mali ya kidunia na matunda ya kazi ya watu.

Kwa ajili ya manufaa ya wote, inadai kujali lengo la wote la mali na heshima ya haki ya mtu kumiliki mali yake. Maisha ya Kikristo yafanya juhudi kupanga mali za ulimwengu huu kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya upendo wa jirani.

(Rejea Katekisimu ya Kanisa Katoliki uk. 524).

Je, kiongozi huyo aliyesema "kupiga haikatazwi' ina maana naye 'alipiga' kwa kiasi chake kwa sababu 'haikatazwi' lakini wenzake 'walipiga mno' kiasi cha kumkatisha tamaa akaona ajiuzulu? Angekuwa na nafasi ya 'kupiga' kama wenzake angejiuzulu? Alichukua hatua gani baada ya kujiuzulu? Au aliona kutoa dukuduku lake gazetini ndio kumaliza tatizo la 'wapigaji' wenzake waliomzidi maarifa?

Aliripoti Takukuru ili taasisi hiyo iwachukulie hatua za kisheria wahusika wote na huyo aliyejiuzulu naye awe shahidi wa upande wa mashtaka? Kama hakuripoti au hajaripoti mpaka sasa ni kwa nini? Kwa upande mwingine watendaji wa Takukuru hawakusoma maelezo ya kiongozi huyo mstaafu baada ya kuona fedha za Yanga 'zinapigwa' (zinaliwa) kupita kiasi hata kumfanya ajiondoe?

Methali ifuatao yawafaa sana wanachama, wachezaji na mashabiki wa Yanga: "Walio chini ya munga sasa wako madarini." Munga ni aina ya mti. Maana yake waliokuwa wakiishi au wakikaa chini ya mti wa munga sasa wanakaa majumbani.

Huweza kutumiwa kutukumbusha kuwa maisha ya watu hubadilika sana. Waliokuwa na hali nzuri na ya kujivunia huenda ikawaondokea; na waliokuwa wanyonge wakafanikiwa.

Vuta hisia hali waliyokuwa nayo Yanga wakati wa Yusuf Manji na sasa Simba ikibebwa na bilionea wao 'MO' Dewji! Ni kama yale yasemwayo na vijana wa mjini "kutesa kwa zamu!" Naam ... ni zamu ya Simba kutesa.

Lahaula! Kumbe aliye juu mngoje chini eh?

**marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096**

## HABARI KITAIFA



Wakazi wa Jiji, wakiwa wamekusanyika wakiperuzi vichwa vya habari kwenye magazeti yaliyokuwa yakiuzwa katika eneo la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Atupwa jela miaka 30 kwa kubaka mtoto

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Itebura Wilaya ya Uvinza, Makigo Maduhu (23), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na kulipa fidia ya Sh. 500,000 kwa kosa la kubaka mtoto wa miaka 13. Hukumu hiyo imetolewa jana na Hakimu wa Mahakama hiyo, Fedrick Shayo, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo bila kuacha shaka.

Hakimu Shayo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo, ili liwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia ya kubaka watoto.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi watano na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo.

Alisema mtoto huyo alifanyiwa kitendo hicho wakati anachunga ndama shambani, ndipo mshtakiwa alimshika kwa nguvu na kumbaka, na baada ya kumbaka alikimbia kusikojulikana na baada ya siku tatu alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Nguruka.

Aidha, alisema mtoto huyo alikwenda nyumbani kuwaambia wazazi wake, ambao walimchukua hadi Kituo cha Polisi Nguruka na kupewa PF3 na kuelekea Kituo cha Afya Nguruka kwa uchunguzi zaidi. Hakimu Shayo alisema alisikiliza ushahidi pande zote na kugundua kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa makusudi, hivyo mahakama kumtia hatiani.

Mshtakiwa huyo alijitetea kuwa anaomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ni kosa lake la kwanza kisha akaangua kilio.

Hakimu Shayo alitupilia mbali utetezi huo na kusema: "Mshtakiwa, kitendo hiki ulichokifanya ni cha kikatili sana, kumshika kwa nguvu msichana mwenye umri wa miaka 13 na kumbaka unaonyesha kuwa wewe ni mzoefu wa vitendo hivi, hivyo basi utakwenda jela miaka 30 na kumlipa msichana huyo fidia ya shilingi 500,000 ili ukajifunze tabia njema na ukimaliza kifungo chako utakuwa raia mwema kwa jamii."

Awali akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Edina Makala, alidai Septemba 15, mwaka 2018, katika Kijiji cha Itebura Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.

# Wadaiwa sugu wakwamisha kampuni binafsi za ulinzi

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

KAMPUNI 54 za ulinzi binafsi zilizopo mkoani Geita zilizoajiri zaidi ya watu 4,500 zinakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo ya ukata wa kujiendesha kutokana na wateja wake kutolipa malipo kwa wakati, hivyo kushindwa kulipa kodi za serikali na mishahara.

Mwenyekiti wa Umoja wa Kampuni Binafsi za Ulinzi Tanzania (TAMASCA) Mkoa wa Geita, Ayoub Chacha Makuruma, alisema hayo juzi, baada ya kumalizika kwa kikao cha kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Geita kilichokuwa pia kimewashirikisha viongozi wa kampuni binafsi za ulinzi na maofisa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA.

Makuruma hata hivyo, alipongeza kuonyesha kuuthamini mchango wa sekta ya ulinzi binafsi baada ya kuhakikishiwa kuwa wateja wote wadaiwa sugu serikali ya wilaya itasimamia kuhakikisha wanalipa kwa wakati kwa mujibu wa mikataba yao ili waweze kulipa kodi za serikali.

Baadhi ya changamoto zilizojadiliwa na serkali ya wilaya kuahidi kuzipatia ufumbuzi ni kufunguliwa kwa ukurasa mpya wa uhusiano kati ya kampuni za ulinzi na TRA kufanya kazi kwa ukaribu ili kuzitatua changomoto zinapojitokeza kabla ya hatua za kisheria ikiwamo faini kuchukuliwa.

Meneja wa TRA Mkoa wa Geita, James Jilala, aliwaambia wamiliki wa kampuni za ulinzi binafsi kuwa TRA inautambua machango wao katika pato la taifa kupitia kulipa kodi, hivyo itaendelea kutoa elimu ya mlipakodi ili kuondoa sintofahamu ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara wakati wa utekelezaji majukumu kwa wateja wao.

Awali baadhi ya wamiliki wa kampuni hizo za ulinzi walimwambia Mkuu wa Wilaya ya Geita, Josephat Maganga, kuwa changamoto kubwa inayowakwamisha ni kwa wateja wao kushindwa kuwalipa kwa wakati kiasi cha kuzifanya kampuni kushindwa kujiendesha ikiwamo kulipa kodi za serikali na mishahara kwa wafanyakazi wake.

Changamoto nyingine ni kutokuwa na elimu ya ulipaji kodi ikiwamo uandaaji taarifa na ukokotoaji wa hesabu za kodi, hatua iliyodaiwa imekuwa ikisababisha kutokea mgongano na mitazamo tofauti kutoka kwa baadhi walipakodi na baadhi ya wamiliki wa kampuni hizo na kujiona kama wanaonewa, lakini baada ya kupatiwa elimu ya mlipakodi sasa wamepata uelewa katika hilo.

# Wanafunzi wapatiwa elimu ya benki

**Na Mary Geofrey**

WANAFUNZI wametakiwa kutumia vyema muda wa masomo kuhakikisha wanatimiza ndoto zao za baadaye ili kuwa sehemu ya kulisaidia taifa kupiga hatua za maendeleo.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NIC, Mick Karima, wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule za Sekondari ya Kisutu na Tambaza walipofanya ziara ya masomo katika benki hiyo kujifunza kazi zinazofanywa hapo.

Alisema wanafunzi ni taifa la kesho ambalo linategemewa katika kufanya shughuli mbalimbali na kuwa viongozi kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchini.

"Nimefurahi sana kupata ugeni wa wanafunzi leo ambao wamekuja kwa ajili ya kujifunza shughuli mbalimbali zinazofanywa na benki hii, naamini wapo wanafunzi hapa watakaokuwa watumishi wa benki siku zijazo," alisema.

Alisema benki hiyo imekuwa ikifanya utaratibu wa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa shule za serikali tangu miaka mitano iliyopita kwa kila mwaka kwa lengo la kuwafunza mambo mbalimbali wanayofanya.

Karima alisema wanafunzi hao wanatembelea idara zote na kuelezwa kila shughuli zinazofanywa na benki hiyo ili kuwajengea uwezo wa kuipenda kazi hiyo.

"Benki ya NIC tunaamini katika kuwaendeleza wanafunzi ambao watakuja kuwa watumishi na wadau wa maendeleo ili wafahamu mapema shughuli tunazofanya katika kuwarahisishia kufikia malengo yao," alisema mkurugenzi huo.

Naye mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Tambaza, Mohamed Mohamed, alisema wamefurahi kushiriki kujifunza kazi zinazofanywa na benki hiyo na kumewafanya kupata ari ya kusoma kwa bidii ili kufikia malengo yao ya baadaye.

"Kwa siku nzima leo tumekuwa hapa benki ya NIC, tumeona namna benki inavyofanya kazi, wanavyohudumia wateja, namna wanavyotoa fedha kupitia mashine lakini pia tumepata fursa ya kuuliza maswali yanayohusu shughuli zao," alisema.

# Tanzania yapata mashine za kisasa kutibu saratani

INATOKA UK. 3

bila malipo kwa Watanzania tu na msiwatoze gharama kubwa za kuwakomoa bali zile za zinazotakiwa ili kutuingizia mapato," alisema Samia.

Pia alisema fedha zitakazopatikana kupitia wagonjwa binafsi na wale wanaotoka nje ya nchi zitawezesha kununua mashine kama hizo ambazo zitafungwa katika hospitali za kanda na mikoa nchini.

Samia pia alihidi kuwa serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya matibabu, ili kuwapunguzia wananchi mzigo wakufuata huduma nje ya nchi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema kuwapo kwa mashine hizo miezi sita sasa, zimesaidia kupunguza muda wa wagonjwa kupigwa mionzi kutoka wiki sita hadi wiki tatu.

Alisema kwa mwaka mmoja pekee wagonjwa 300 walikuwa wanaenda rufani nje ya nchi hasa India kwa ajili ya kupata tiba, ambapo mgonjwa mmoja hugharimu Sh. milioni 50 ikiwamo tiba ya mionzi, malazi na usafiri.

Ummy alisema katika katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita wagonjwa wapya wa saratani 13,400 walikuwa wakihudumiwa katika taasisi ya Ocean Road, Bugando, Muhimbili, KCMC na hospitali binafsi ambao ni sawa na asilimia 31.9 ya wagonjwa wote wa saratani nchini.

Waziri huyo alisema katika kipindi chake cha uongozi amesaidia upatikanaji wa dawa katika taasisi hiyo kutoka asilimia nne mwaka 2015/16 hadi asilimia 92 Februari 2019 kwa wagonjwa wa msamaha.

Alisema upatikanaji wa dawa kwa mwezi Oktoba mwaka 2018 ulifika asilimia 95. "Hii haijawahi kutokea katika nchi za uchumi wa hali ya chini kama Tanzania," alisema.

Kwa mujibu wa Ummy, idadi ya wagonjwa katika hospitali hiyo imeongezeka kwa kuwa awali wagonjwa walihofia kwenda kwa sababu ya changamoto za upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, msongamano wa wagonjwa na kukosa tiba kwa wakati.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ORCI, Dk. Julius Mwaiselage, alisema awali serikali ilitenga Sh. bilioni 14 kwa ajili ya ununuzi wa mashine hizo za kisasa kupitia wakala, lakini wakaagiza moja kwa moja kwa kutoka kiwandani na kupatikana kwa Sh. bilioni 9.5 kulikosaidia kuokoa Sh. bilioni 4.5.

Alisema gharama za ujenzi wa jengo na ununuzi wa mashine hizo ni fedha za serikali kwa asilimia 100.

Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa ya Utafiti wa Saratani (IARC) ya Septemba mwaka 2018, Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya 42,060 na takribani wagonjwa 28,620 hufariki kwa mwaka.

Pia inakadiriwa kuwa vifo vitokanavyo na saratani vinatarajiwa kuongezeka na kufikia milioni 24 ifikapo mwaka 2035 kama juhudi za kinga na tiba hazitaimarishwa katika nchi hizo.

# Ofisa usalama ashtakiwa kesi ya uhujumu uchumi

INATOKA UK. 4

Ng'itu anakabiliwa na mashtaka 12 ya uhujumu uchumi na moja la kughushi nyaraka.

Tibabyakoma alidai kuwa Juni 20, 2016, Ng'itu akiwa wilayani humo eneo lisilojulikana, alijipatia Sh. milioni moja malipo yasiyo halali kutoka kwa mkurugenzi wa OBC, huku akijua kampuni hiyo ina maslahi na mgogoro wa Pori Tengefu la Loliondo, hivyo alikuwa na kila sababu ya kujua mgogoro huo una uhusiano na kazi yake.

Aliendelea kudai kuwa katika shtaka la pili, la tatu, la nne, la tano, la sita, la nane, la tisa, la 10, la 11 na kwa tarehe tofauti tofauti kati ya Septemba 2, 2016 hadi Julai 15, 2017, Ng'itu alijipatia manufaa bila malipo halali Sh. milioni tisa kinyume cha sheria kutoka kwa Mkurugenzi wa OBC, huku akijua kulikuwa na kila sababu ya kuamini kampuni ya OBC ilikuwa na maslahi katika mgogoro wa Pori Tengefu la Loliondo matumizi mseto ya ardhi, huku akijua kabisa mgogoro huo ulikuwa na uhusiano na kazi yake.

Aidha, Tibabyakoma aliendelea kudai kuwa Machi 14, 2017, Ng'itu akiwa wilayani Ngorongoro eneo lisilojulikana, alijipatia Sh. 5,550,000 kutoka kwa mkurugenzi huyo wa OBC huku akijua kampuni hiyo ina maslahi makubwa katika mgogoro huo wa pori tengefu na kwamba mgogoro huo ulikuwa na uhusiano wa kazi yake.

Tibabyakoma pia alidai kuwa kati ya Machi 14, 2017 katika eneo lisilojulikana jijini Dar es Salaam, Ng'itu na Mollel walighushi nyaraka ya mkataba wa mauzo wa gari aina ya Land Cruiser Prado lenye namba za usajili T 456 DFZ mali ya Mkurugenzi wa OBC na kumuuzia Ng'itu kwa Sh. milioni mbili.

Aliendelea kuileza mahakama hiyo kuwa baada ya kughushi mkataba huo Machi 14, 2017 mkurugenzi huyo wa OBC alichukua mkataba huo na kuupeleka Mamlaka ya Mapato (TRA) Wilaya ya Ilala kwa lengo la kuiaminisha mamlaka hiyo kuwa ameuza gari hilo kwa Ng'itu kwa thamani ya Sh. milioni mbili jambo ambalo si kweli.

Pia alidai kuwa kati ya Desemba, 2018 na Februari 2019 katika Jiji la Arusha, Mkurugenzi huyo wa OBC na Ng'itu waliwasilisha mkataba wa kughushi uliokuwa umeandikwa Machi 11, 2017 uliokuwa unaonyesha kuwa Mollel amemuuzia Ng'itu gari hilo aina ya Toyota Land Cruiser Parado lenye namba za usajili T 456 DFZ kwa thamani ya Sh. milioni 27, wakati wakijua kuwa si kweli kwa sababu gari hilo liliingizwa nchini na Mollel likiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 51.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Hakimu Bwegoge aliwataka watuhumiwa hao kutojibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na kuhoji mawakili wa utetezi, Daudi Haraka aliyekuwa anayemtetea Mollel na Charles Mollel anayemtetea Ng'itu kama wana hoja yoyote ya kuwasilisha mahakamani hapo.

Mawakili hao waliuomba upande wa Jamuhuri kuharakisha upelelezi na kutokana na majibu hayo, Hakimu Bwegego alihoji upande wa Jamuhuri kama upelelezi umekamilika na Tibabyakoma akadai kuwa wanaomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kuwa sababu upelelezi haujakamilika.

Kutokana na majibu hayo, hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 11, mwaka huu na kuamuru watuhumiwa wote wapelekwe mahabusu ya Gereza Kuu la Kisongo.

# Asimulia alivyookolewa ndoa utotoni

INATOKA UK. 3

"Tangu siku hiyo nilipookolewa kuozeshwa ndoa ya utotoni, baba yangu alinifukuza nyumbani na hataki hata kuniona hadi leo.

Kwa sasa nalelewa na shirika hili la Agape pamoja na kusoma kwenye shule yao ya sekondari ya mfumo wa elimu ya watu wazima ili kutimiza ndoto zangu," aliongeza.

Baadhi ya madiwani hao, akiwamo Stimar John kutoka Kata ya Ijombe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, walisikitishwa na vitendo hivyo vya wazazi kupenda kuozesha wanafunzi na kuwakatisha masomo yao na kuomba elimu itolewe zaidi kwa jamii juu ya madhara ya ndoa za utotoni.

Meneja Mradi wa Kutokomeza Mila na Desturi kutoka Agape, Amani Peter, akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, John Myola, alisema walianzisha shule hiyo ili kutimiza ndoto za waathirika wa mimba na ndao za utotoni.

Alisema waathirika hao baada ya kuwaokoa, wazazi wao huwakataa ndipo wao huchukua jukumu la kuwatunza kwa kufuata sheria serikalini na kuamua kuwasomesha.

Peter alisema kwa mwaka jana katika shule hiyo, wanafunzi 29 walifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne na kati yao 12 walipata daraja la tatu, 17 daraja la nne na wanaendelea na masomo.

# Upelelezi kesi vigogo Barrick

INATOKA UK. 3

11, 2008 na Juni 30,2007 katika sehemu tofauti za Jiji la Dar es Salaam, Kahama mkoani Shinyanga, Tarime (Mara) na Biharamulo mkoani Kagera maeneo ambayo yako katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Maeneo mengine ambayo washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo ni katika mji wa Johannesburg, Afrika Kusini, Toronto (Canada) na Uingereza.

Aidha, Mwanyika na Lugendo wanadaiwa kutoa msaada katika kusimamia mkakati wa kihalifu kwa nia ya kupata faida.

Washtakiwa hao wanadaiwa kutoa tamko la uongo kwa Kamishna Mkuu wa TRA huko Biharamulo kwa nia ya kukwepa kulipa kodi Dola za Marekani, 9,309,600 ambayo ilipaswa kulipwa TRA.

Pia Mwanyika na Lugendo wanadaiwa kuwa kati ya Desemba, 2009 na Desemba 31, mwaka jana katika maeneo tofauti ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa pamoja na wengine ambao hawapo mahakamani, walisaidia mgodi wa North Mara kuhamisha Dola za Marekani, 374,243,943,45, huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la makosa ya kughushi na kukwepa kodi.

Pia washtakiwa wanadaiwa kati ya Novemba 2, 2012 na Novemba 27, 2015 huko Shinyanga walitoa rushwa ya Sh. 718,520,001.76 kwa Hussein Kashindye ambaye ni Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa (RCO) wa Shinyanga kwa lengo la kumshawishi ili aachane na uchunguzi wa makosa ya jinai yaliyokuwa yametendwa na mgodi wa Bulyanhulu.

Katika shtaka la kughushi, washtakiwa hao wakiwa na nia ya ulaghai, wanadaiwa walighushi mkataba wa mkopo wakitaka kuonyesha kwamba Aprili 30, 2014 Kampuni ya Pangea Limited ilikubali kukopa USD 90,000,000 ikiwa na riba kutoka benki ya kimataifa ya Barrick, huku wakijua kuwa si kweli.

Katika shtaka la kutoa nyaraka ya uongo, Mwanyika anadaiwa kuwa Aprili 30, mwaka jana katika Benki Kuu ya Tanzania, Ilala jijini Dar es Salaam, kwa makusudi aliwasilisha nyaraka ya uongo ya mkopo baina ya kampuni mgodi wa Bulyanhulu na Barrick International Bank Corp kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa, kati ya Juni 2001 na Desemba 13, 2007 Bulyanhulu walijipatia mkopo usio na faida wa Dola za Marekani, 416,100,000 kutoka Barrick.

# Nassari akwaa kisiki mahakamani

INATOKA UK. 2

Kutokana na ombi hilo, mahakama hiyo ilizuia kutofanyika uchaguzi mdogo wa ubunge Arumeru Mashariki hadi shauri hilo litakapoamuriwa.

Machi, 14 mwaka huu, Bunge lilitangaza kuwa mbunge huyo amepoteza sifa ya ubunge wake baada ya kutohudhuria mikutano ya bunge mitatu mfululizo.

Mikutano ambayo hakuhudhuria ni mkutano wa 12 wa Septemba 4 hadi 14, mwaka jana, mkutano wa 13 wa Novemba 6 hadi 16 na mkutano mwaka 2018 na hakuhudhuria mkutano wa 14 uliofanyika kuanzia Januari 29 hadi Februari 9, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na bunge, uamuzi huo umezingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 71 (1) (c).

Ibara hiyo inaeleza kuwa: "Mbunge atakoma kuwa mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge ikiwa atakosa kuhudhuria vikao vya mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ruhusa ya Spika.

Pia ibara hiyo imefafanuliwa katika Kanuni ya 146 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 kuwa: "Kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake ni wajibu wa kwanza wa Mbunge. Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ruhusa ya Spika iliyotolewa kwa maandishi, atapoteza ubunge wake na Spika ataiarifu NEC."

## HABARI ARUSHA

# Diwani awachongea vigogo wa CCM kwa Pinda kuhodhi ardhi

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

DIWANI wa Kata ya Maisaka, Abdulaman Kololi, amewashtaki kwa Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Mbunge Andrew Chenge (CCM), na aliyewahi kuwa Mbunge wa Arusha mjini, Felix Mrema (CCM), kwa kumiliki ardhi kubwa katika kijiji cha Malangi, huku wananchi wanakosa maeneo ya kulima.

Aliwasilisha mashtaka hayo katika kijiji cha Malangi, alipopewa nafasi ya kusalimia wananchi wake kwenye mkutano wa hadhara uliokuwa umeandaliwa kwa ajili ya kumpokea Pinda ambaye alikuwa kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, (CCM), pia ambaye ni mlezi wa Mkoa wa Manyara wa chama.

Kololi alimwomba Pinda kumsaidia kupata hatima ya shamba la Tina Estate lililoko kijijini hapo ambalo linadaiwa kufutwa kwa mujibu wa taarifa za Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Mji wa Babati, huku akisema wakati mwingine wataalamu wa ardhi wanakanusha kuwa shamba hilo halijafutwa ni mali ya Chenge na Mrema. "Kutokana na mimi nilikuwa Chadema sijui vizuri, lakini taarifa nilizozipata shamba hili lilishafutwa na alipokuja Waziri wa Ardhi, William Lukuvi, mwanzoni mwa mwezi huu, wataalamu wa ardhi walisema limefutwa ila ukiwafuata tena wanasema halijafutwa naomba unisaidie," alisema.

"Nilipokuwa Chadema nilionekana kwa wananchi kama mhuni maana sikuwa ninashirikiana na serikali na sasa nimerudi CCM nisije nikaonekana kama mhuni tena naomba mlezi unisaidie shamba lifutwe na watu wangu wapate eneo la kulima," alisema.

Aidha, alisema shamba hilo lina ukubwa wa zaidi ya heka 3,000 na vigogo hao wamekuwa wakiwatumia watu kuwakodishia shamba hilo ambapo kwa heka moja inakodishwa kwa Sh. 50,000 tu na hivyo kuwafanya wananchi ambao hawana uwezo wakose maeneo ya kulima.

Wataalamu wa ardhi waliokuwa kwenye mkutano huo walipoulizwa juu ya shamba hilo walishindwa kutoa maelezo ya kuondoa utata huo ambao unawaumiza wananchi kwa kukosa mahali pa kulima na ndio maana wananchi walipokea msafara wa Pinda kwa mabango yaliyokuwa yanadai shamba hilo kurejeshwa.

Akijibu hoja za diwani huyo, Pinda alisema hilo siyo tatizo kubwa na aliwaagiza wataalamu wa ardhi kulifanyia kazi suala hilo ndani ya wiki mbili liwe limeisha ili kama ni shamba kufutwa lifutwe wapewe wananchi wafanye shughuli zao.

Alisema mtu kama anamiliki ardhi halafu anashindwa kuliendeleza zipo taratibu za kufuata zikikamilika Rais ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kufuta mashamba pori anayafuta na kurudisha kwa wananchi.

Alitumia fursa hiyo kumtaka diwani huyo kuendelea kufuatilia jambo hilo na kama wataalamu wa ardhi watashindwa kulimaliza tatizo hilo ndani ya wiki mbili akusanye nyaraka zote na kuzipeleka Dodoma kwa watu ambao wanahusika ili wazifanyie kazi haraka.

Baada ya Waziri Mkuu mstaafu huyo kutoa maelekezo, wananchi walishangilia kwa kupiga makofi na nderemo wakiashilia kukubaliana na maelekezo aliyoyatoa kwa mamlaka zinazohusika na masuala ya ardhi.



Katibu wa CCM Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Ally Kidunda, akipandisha bendera ya chama hicho wakati akizindua shina la wakereketwa la Lameck Mwakisole, Songambele sokoni juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ushirikiano wa mahakama kuondoa vita tafsiri za kisheria

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, (AfCHPR), imesema misingi mizuri ya ushirikiano inayoendelea kujengwa na Mahakama ya Afrika Mashariki, (EACJ), inawapa uhakika wa kutokuwa na 'vita' ya tafsiri ya masuala ya kisheria kati ya taasisi hizo mbili.

Rais wa mahakama hiyo, Jaji Sylvain Ore, alisema hayo wakati Rais wa EACJ, Jaji Dk. Emmanuel Ugirashebuja, alipotembelea Mahakama ya Afrika hivi karibuni.

"Tuna uhakika kwamba sasa, hakutakuwa na vita ya tafsiri za kisheria na badala yake wote wanafanya kazi moja ya kulinda haki za binadamu kwa kila mmoja," alisema. Alisema kwa ujumla mahakama hizo zinazingatia kwa umoja wao haki za kiuchumi, kijamii, kiraia na kisiasa.

Aliongeza kuwa ushirikiano wao umekuwa wa mafanikio kati yao akitaja uwekaji wa mfumo wa teknolojia ya kisasa wa kimahakama, uchukuaji wa ripoti na uwekaji wa mifumo ya sauti katika mwenendo wa kesi mahakamani.

Mafanikio mengine ni ushirikiano wa kubadilishana mawazo na utekelezaji wa miradi inayoendeleza kati ya taasisi hizo kama vile midahalo ya kisheria,

Mtandao wa Kimahakama wa Afrika, kuendeleza elimu ya sheria, kuwa na mipango kazi ya haki za binadamu.

# Wachimba madini wajipanga kuanzisha benki

**Na Mwandishi Wetu,** MIRERANI

CHAMA cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara, (Marema), kimeshauri vyama vya wachimbaji madini vya mikoa kuanzisha vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa (Saccos) ili kuwezesha uanzishaji wa benki ya wachimbaji madini.

Mwenyekiti wa Marema, Justin Nyari, alitoa ushauri huo Mirerani, wilayani Simanjiro juzi, wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya wadau wa madini iliyoandaliwa na Tume ya Madini.

Alisema wachimbaji madini wa kila mkoa wakianzisha Saccos yao wataweza kujisimamia na kujiwezesha zaidi kiuchumi hadi kuanzisha benki yao.

Aliongeza kuwa endapo kila mkoa utaanzisha Saccos yao itakuwa bora zaidi kwenye usimamizi kuliko kuwapo na moja ya wachimbaji nchi nzima.

Mwenyekiti wa Tanzanite, Money Yousuph, alisema kupitia shirikisho la wachimbaji madini nchini, (Femata), wanatarajia kukutana mkoani Shinyanga, Machi 30, mwaka huu, kwa ajili ya uanzishwaji wa Saccos hiyo.

Alisema kupitia Saccos na kuanzisha benki yao watafanikisha kujikopesha vipuli vya migodini na gharama za milipuko.

Mhandisi wa Migodi kutoka Tume ya Madini, Laurent Mayala, alisema suala la uanzishaji Saccos litawasaidia wachimbaji hao kwa kuwa hivi sasa ruzuku imesitishwa.

"Serikali imeamua kusitisha kwa muda hili suala la utoaji ruzuku kwa wachimbaji baada ya kuona mambo yanakwenda ndivyo sivyo kwenye utoaji wa ruzuku kwa wachimbaji," alisema.

Mmoja kati ya wachimbaji wa madini ya tanzanite, Charles Enock, alisema suala la uanzishwaji wa Saccos litakuwa ni mkombozi kwa wachimbaji madini hususani wa tanzanite.

"Hivi sasa sisi wachimbaji madini inakuwa vigumu kukopesheka ila tukiwa na benki yetu tunaweza kufaidika kwa kujikopesha na kurudisha mikopo," alisema.

Mchimbaji mwingine, Mwanaidi Kimu, alisema wachimbaji madini wanapaswa kuungana na serikali katika shughuli zao.

"Hivi sasa wachimbaji madini tupo kifua mbele kwa kuwa Rais John Magufuli anatupenda na alituita tukakutana naye akatusikiliza na kuondoa kero mbalimbali," alisema.

Mafunzo hayo yaliyowashirikisha wadau wa madini 150 yalifunguliwa na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula.

# Mwalimu asakwa tuhuma kumpa mimba mwanafunzi

**Na Paul William,** HAI

POLISI mkoani Kilimanjaro, inamsaka Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Sawe iliyoko Wilaya ya Hai ambaye anakabiliwa na tuhuma ya kumpachika ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi Hamisi Issah, amethibitisha kuwa jeshi hilo kwa sasa linamsaka mwalimu huyo kwa udi na uvumba, baada ya kudaiwa kutokomea kusikojulikana.

"Ni kweli hilo tukio limeripotiwa na tunamtafuta lakini siwezi kulizungumzia kwa sasa kwa sababu ya upelelezi," ameeleza Kamanda Issah.

Baada ya taarifa hizo kuzagaa, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya ambaye pia ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, alisema kwa mwaka huu peke yake, mwanafunzi huyo ni kati ya wanafunzi watatu waliokatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito wakiwa shuleni.

"Jumla ya wanafunzi watatu katika Shule ya Sekondari ya Sawe, wamefukuzwa shule baada ya kugundulika kuwa ni wajawazito. Wanafunzi waliofukuzwa shule ni wa kidato cha pili, tatu na nne," amesema Ole Sabaya.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, baada ya polisi kupokea taarifa hizo za mwalimu huyo, Machi mosi, mwaka huu, saa 10:00 jioni, walikwenda shuleni hapo na kukuta mwalimu huyo ameondoka na kwenda kusikojulikana na mpaka sasa hajulikani alipo.

Alipotafutwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sawe, Emmanuel Mushi, akizungumzia mdai hayo, alisema wanafunzi wa kike katika shule hiyo kupewa ujauzito ni matendo yasiyokubalika na ni fedheha kubwa kwao na hivyo akatoa rai kwa vyombo vya dola kuongeza juhudi kuwasaka wote waliohusika.

Mkuu wa shule hiyo, Cecilia Kulawa, ameeleza kuwa makamu mkuu wa shule hiyo alitoweka tangu Machi mosi mwaka huu na kwamba mpaka sasa hawana taarifa zake mahali alipo.

Alisema wanafunzi watatu wa kidato cha pili, tatu na nne, waligundulika kuwa ni wajawazito Februari 28, mwaka huu na kusimamishwa kuendelea na masomo.

Kikao cha Bodi ya Shule hiyo kilichofanyika Machi 22, mwaka huu, kiliridhia kufukuzwa shule kwa wanafunzi hao.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Reli Juu, iliyopo wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro, ambao wamepatiwa mafunzo na Shirika lisilo la kiserikali la Action for Justice in Society (AJISO), juu ya masuala ya ukatili kwa watoto pamoja na haki zao wakiwa na Mkuu wao wa Shule, Idrisa Mkindi, pamoja na wafanyakazi wa shirika hilo, baada ya mafunzo hayo jana. Mradi huo unalenga kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. **PICHA: JAMES LANKA**

# Sumu yasambaratisha mradi wa samaki

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIJANA 16 walioanzisha mradi wa kiuchumi wa ufugaji wa samaki katika kijiji cha Magadini, Wilaya ya Hai, wamepata hasara ya zaidi ya Sh. milioni 2.7 kutokana na sumu iliyowekwa katika chanzo kimoja cha maji na kusababisha vifo vya samaki na udumavu kwa samaki wengine.

Hasara pamoja na hujuma hiyo vilijulikana jana, baada ya wajumbe wa kamati ya utekelezaji ya Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Kilimanjaro kuzuru eneo la mradi huo wa vijana kuona changamoto zao na namna unavyotekelezwa.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Magadini Vijana Group (MVG), Godlisten Cuthbert, aliwaeleza wajumbe hao kuwa vifo vya samaki hao vilitokana na sumu iliyotoka kwenye gari moja lililokuwa likioshwa kwenye chanzo cha maji yanayotiririka kuelekea kwenye bwawa lenye mradi huo na kusababisha samaki wengine kudumaa.

"Mheshimiwa Katibu wa Mkoa wa UVCCM (Abdulrahim Hamid) na wajumbe uliofuatana nao, tunakuomba utusaidie kufuatilia suala hili kwa sababu kuchelewa kwa majibu ya aina ya sumu iliyotumika kuua samaki hao kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

"Tangu Desemba 14, mwaka jana, mpaka leo hii hatujapata majibu na tayari tumepata hasara ya zaidi ya shilingi milioni 2.7 gharama za uendeshaji wa mradi wa samaki ni kubwa kuliko kipato tulichonacho, tunaomba ikiwezekana tuwezeshwe zaidi ili kufikia malengo ya uwekezaji wa mradi huu... Tumeshindwa kurejesha marejesho ya mkopo tuliopewa na Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Baada ya maelezo hayo, Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Hai, Cedrick Pangani, alieleza kuwa pamoja na juhudi kubwa za vijana hao kujitafutia kipato kupitia mradi huo, wana kila sababu ya kuiomba tena serikali pamoja na Halmashauri ya Wilaya hiyo iwawezeshe zaidi katika mradi huo kwa kuwa una faida kubwa kwa wakazi wa wilaya hiyo.

Alipoitwa kutoa ufafanuzi kuhusu mradi huo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Lucas Msele, alisema vijana hao wanaojituma kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi, kabla ya kuanza mradi huo walijichangisha wenyewe kiasi cha Sh. milioni saba na halmashauri ikawapa mkopo wa vijana wa asilimia 4 kiasi cha Sh. milioni tatu.

Hata hivyo, wakati anajibu ombi la vijana hao, Katibu wa UVCCM mkoa wa Kilimanjaro, Abdulrahim Hamid, alisema iko haja kwa serikali kuu na halmashauri za wilaya kuangalia uwezekano wa kuanza kuiwekea bima, mikopo yote inayotolewa kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na walemavu.

"Hili la kuchelewa kwa majibu ya sumu tumelipokea na tutawasiliana na ofisi ya DC (Mkuu wa Wilaya ya Hai) na chama kuona namna linavyoweza kupata ufumbuzi. Ofisa Maendeleo ya Jamii uliyeko hapa, nadhani mnapaswa kuona umuhimu wa kuiwekea bima mikopo hii maana kama hawa vijana wangekuwa na bima, hata hiyo hasara wanayolalamikia isingekuwapo," alieleza Abdulrahim.

## DC 'atia mguu' sakata la mgogoro wa shamba

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI katika Wilaya ya Hai, imetangaza kuzirejesha kwa wananchi ekari 112 za ardhi ambazo ni mali ya wanachama wa Chama cha Ushirika wa Mazao cha Lyamungo AMCOS ambazo zilikuwa ziuzwe kwa Sh. milioni 500 ili kufidia mkopo wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoa wa Kilimanjaro (KNCU).

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akizungumza na wananchi wa Kata ya Machame Mashariki, wilayani humo alisema haki ya shamba hilo iko kwa wanachama wa Lyamungo Amcos na siyo KNCU.

"Shamba hili naamini ni mali yenu ambalo mlinunua kwa fedha za mkopo kiasi cha Sh. 200,000 na mlianza kwa kulipa deni hilo mara ya kwanza 158,000 awamu ya pili mlilipa kiasi 11,460 na awamu ya tatu mkalipa kiasi 8,600. Naamini kabisa mlilipa deni kwa asilimia 90 na deni lililokuwa limebaki lilikuwa ni kiasi cha Sh. 12,000 ambazo nazo mlilipa kupitia KNCU kwa kukatwa fedha wakati wa kuuza kahawa," alisema Ole Sabaya. Wananchi ambao ndiyo wamiliki wa chama hicho cha ushirika wa mazao cha Lyamungo Amcos walikuwa katika mgogoro kwa zaidi ya miaka 16 sasa. Shamba hilo lililopo katika Kata ya Machame Mashariki, linadaiwa kumilikiwa na chama hicho baada ya kununua kutoka kwa raia wa Ugiriki, Philip Filios, baada ya kuliuza kwa njia ya mnada.

Ole Sabaya ameeleza kuwa uamuzi huo wa serikali umefikiwa, baada ya kudaiwa kuwa eneo hilo limepokwa na Chama Kikuu cha Ushirikia mkoani Kilimanjaro (KNCU) kinyume na taratibu.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwanasheria wa Halmashauri hiyo, Henglibert Boniface, alisema amepitia nyaraka zote zilizowasilishwa katika ofisi za halmashauri na kwamba ofisi yake imejidhirisha kuwa kuna ujanja umefanywa na KNCU ili kuwadhulumu wanachama hao shamba hilo. Awali akisoma taarifa yao kwa Ole Sabaya, Mwenyekiti wa Chama hicho cha Lyamungo AMCOS, Gabriel Ulomi, alisema madhara ya mgogoro wa shamba hilo ni pamoja na kupata hasara kubwa kutokana na kusimama kwa shughuli za uzalishaji kwa zaidi ya miaka 16, baada ya chama kulazimika kuweka zuio mahakamani.

"Mkopo wa Sh. milioni 500 haukuhusisha Lyamungo Amcos na wala hakukuwapo madai yoyote ambayo KNCU ilikuwa ikidai Chama cha Lyamungo, japo Lyamungo Amcos ilihusika kuiomba serikali ilipe deni hilo ili kunusuru shamba letu lisiuzwe, tunaishukuru sana serikali kwa kulipa deni hilo.





Wachuuzi wakiwa wametandaza bidhaa zao chini wakati wakisubiri wateja katika makutano ya Mtaa wa Utete na Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala Sokoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yatoa fursa kwa waliofaulu kidato cha tano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema zoezi la kuchagua wanafunzi kujiunga kidato cha tano au chuo litafanyika baada ya kubadili tahasusi au kozi walizochagua awali ili wasome wanachokitaka.

Hatua hiyo imetokana na baadhi ya wanafunzi kutojaza kwa uhakika tahasusi zao kwa kutokuwa na uhakika wa ufaulu katika masomo yao.

Waziri wa Nchi, Tamisemi, Seleman Jafo, akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, alisema serikali imetoa fursa hiyo kwa wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2018 kufanya mabadiliko hayo kwa kozi walizochagua kwenye fomu ya 'F4-Selform'.

"Fursa hii itawawezesha wanafunzi kurekebisha machaguo yao kulingana na ufaulu waliopata kwenye matokeo ya kidato cha nne 2018 yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA),"alisema.

Alibainisha kuwa wanafunzi hao watakuwa na uwezo wa kubadili machaguo au kuchagua kutoka kidato cha tano kwenda chuo au chuo kwenda kidato cha tano.

Jafo alifafanua kuwa fursa hiyo inatoa mwanya kwa mwanafunzi kusoma fani itakayomwandaa kuwa na utaalamu fulani katika maisha yake ya baadaye kwa namna ambayo anatamani yeye mwenyewe au kwa kushauriwa na wazazi au walezi wake.

"Hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya wanafunzi hawakujaza kwa uhakika tahasusi zao, zoezi la awali la kuingiza taarifa zilizo kwenye Selform za wanafunzi kwenye kanzidata ya ofisi ya Tamisemi kama zilivyojazwa wakiwa shuleni lkabla ya kuhitimu limekamilika," alisema.

Waziri huyo alisema wanafunzi hao watabadili kwa njia ya mtandao kadri watakavyotaka na baada ya kufanya marekebisho hayo kanzidata hiyo itatumika kuwapanga kidato cha tano na kozi za vyuo.

"Wanafunzi watumie anuani ya www.selform.tamisemi.go.tz na maelekezo ya jinsi ya kufanya mabadiliko yanapatikana kupitia Youtube video inayopatikana kwenye tovuti ya Tamisemi ya www.tamisemi.go.tz," alisema.

Kadhalika, alisema ili mhitimu aweze kuingia kwenye mfumo itabidi kutumia namba ya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka 2018, jina lake la mwisho, mwaka wa kuzaliwa na alama ya ufaulu aliyopata kwenye somo atakaloulizwa na mfumo au swali lolote litakaloulizwa.

Jafo alisema zoezi hilo litafanyika kuanzia Aprili mosi hadi Aprili 15, mwaka huu.

Hata hivyo, alisema baada ya zoezi hilo ofisi yake haitapokea maombi ya kubadili tahasusi na ambaye hatabadili taarifa zake kwa kipindi husika Tamisemi itaamini mwanafunzi ameridhika na machaguo yake.

# Walengwa wa Tasaf wakumbushwa umakini

**Na Elisante John,** SINGIDA

IMEELEZWA kuwa changamoto za kipato kwa kaya maskini zaidi nchini zinaweza kupungua, iwapo walengwa watazingatia elimu wanayoipata kabla na baada ya kupokea fedha zinazotolewa na mfuko wa maendeleo ya jamii nchini (TASAF).

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mratibu wa mfuko huo Juma Nzogu, alipokutana na walengwa hao kwenye vituo vya kutolea ruzuku, vilivyopo kwenye mitaa na vijiji mbalimbali vya Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Nzogu aliwataka walengwa kutumia vema fedha wanazopata, kwa maslahi ya familia zao, sambamba na kuanzisha miradi ya kiuchumi, itakayowaongezea kipato, na hivyo kuepuka aibu ya kuitwa maskini, baada ya muda wa mpango wa Tasaf kumalizika.

Aidha, aliwaasa wanafunzi wasichana wa rika la balehe, walio kwenye mpango huo kutoka kaya maskini wanaonufaika na fedha pia taulo za kike, kuongeza bidii ya masomo darasani. Pia Nzogu aliwataka walengwa hao kutumia vema fedha za ruzuku, ili kuendana sawa na taratibu walizoelekezwa na wataalamu, ikiwamo kununulia mahitaji ya shule kwa ajili ya elimu kwa watoto wao na kuwapeleka kliniki watoto wadogo, bila ya kusahau kujiwekea akiba kwa maisha yao ya baadaye.

Mmoja wa walengwa Mwanahamisi Shabani alipongeza serikali juu ya mpango huo, huku akiomba fedha za ruzuku ziongezwe.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo, alisema kiasi cha Sh. milioni 178.6 kimetolewa kwa ajili ya walengwa 2,823 waliopo kwenye vijiji na mitaa 27 ya Manispaa ya Singida.

Pia alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 73.8 ni kwa ajili ya wasichana 1,291 wanaotoka kaya maskini zaidi.

# Wauguzi wapewa mafunzo kupunguza vifo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAUGUZI wa afya 50 kutoka katika vituo 25 vya Halmashauri ya Jiji la Dodoma wamepatiwa mafunzo ya huduma ya mama na mtoto ili kuweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi nchini.

Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa katika vizazi hai 100,000, vifo ni 556 na katika watoto wanaozaliwa 1,000 vifo ni 26 kwa mwaka.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Charles Kiologwe, alisema vifo vya kinamama na watoto vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto kubwa nchini.

Alisema kupitia mafunzo hayo yaliyotolewa kwa ufadhili wa Kanisa la Yesu Krito la Watakatifu wa Siku za Mwisho, anatumaini kuwa wahudumu hao watakwenda kuyafanyia kazi ili kupunguza idadi hiyo ya vifo.

Dk. Kiologwe alisema kuwa Tanzania haijaweza kufikia malengo ya melenia katika kupunguza vifo vya kinamama na watoto vitokanavyo na uzazi pamoja na juhudi zilizofanywa na serikali.

"Pamoja na takwimu hizi zilizopo, lazima sisi tuende mbele zaidi kwa kuwa hii takwimu vifo 556 hata kama ingekuwa vifo 20 kwa mwaka, bado ni tatizo kwa sababu wale wanaokufa ni watu ambao walitakiwa kuendelea kuishi, hivyo basi tuhakikishe kuwa tunatimiza wajibu wetu," alisema.

Aliwataka wahudumu hao watakapo rudi katika vituo vyao vya kazi wahakikishe kuwa wanatengeneza timu ambazo zitaweza kupunguza vifo hivyo.

"Lazima mkitoka hapa mwende kuyafanyia kazi mafunzo haya ambayo mmeyapata na siyo kwenye kuukalia huu ujuzi ambao mmeupata katika siku ambazo mlikuwapo hapa," alisema.

Naye Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anatolia Mkindo, alisema kuwa mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kuwa vifo vya kinamama na watoto nchini vinapungua.

"Mafunzo haya kwa mara ya mwisho nakumbuka yalitolewa mwaka 2007, hivyo wahudumu wengi walikuwa hawana ujuzi huu wa kuwasaidia watoto kupumua na mama kuishi," alisema.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yatasaida hasa kwa Mkoa wa Dodoma ambao hivi sasa haufanyi vizuri katika suala hilo la vifo vya kinamama na watoto vitokanavyo na uzazi.

"Mkoa wetu haufanyi vizuri kwa mwaka jana vifo vya uzazi vilikuwa zaidi ya 500 na watoto ilikuwa ni zaidi ya 60, hivyo jitihada bado zinahitajika," alisema.

Kadhalika, Mratibu wa Mradi huo wa Huduma ya Mama na Mtoto, Dk. Ipiana Mwampagatwa, alisema kuwa pamoja na kutoa mafunzo hayo pia wanawapatia washiriki vifaa tiba kwa ajili ya kinamama na watoto.

"Vifaa hivi vitakwenda kutumika katika maeneo yao, lakini pia itakuwa ni sehemu ya wao kuwafundishia wenzao ambao hawakupata mafunzo haya ili waweze kujifunza na kupunguza vifo hivi katika maeneo yao," alisema.





# Spika Ndugai achekelea utekelezaji wa Ilani ya CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Job Ndugai, amesema amefurahishwa na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020 unaofanywa na Serikali ya Zanzibar.

Ndugai ambaye ni mlezi wa CCM Unguja alisema hayo huko Bambi Wilaya ya Kati Unguja wakati aliposhiriki kazi za ulazaji wa mabomba ya majisafi na salama hadi Kijiji cha Uroa ikiwa ni sehemu ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo ambalo limedumu kwa muda mrefu.

Alisema huduma za majisafi na salama pamoja na ujenzi wa miradi ya huduma za jamii ikiwamo shule pamoja na zahanati ndiyo mikakati inayohitajika.

"Nimefurahishwa na kuridhika na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM unaofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo matumaini yangu makubwa malengo yatafikiwa hata kabla ya mwaka 2020 kutokana na kasi ya serikali na viongozi wenyewe wa majimbo," alisema.

Aidha, Ngugai alisema ameridhishwa na matumizi mazuri ya fedha za mfuko wa jimbo wanazopatiwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kusaidia huduma na utekelezaji wa miradi ya jamii katika jimbo.

Aliwataka viongozi wa CCM kufuatilia fedha hizo na kuhakikisha zinatumika vizuri kwa ajili ya maendeleo ya jimbo na kuzipatia ufumbuzi kero za wapigakura.

"Nimefurahishwa na utekelezaji wa Ilani ya CCM katika mambo yote ya msingi ya huduma za jamii, ambapo miradi ya shule inaongoza katika majimbo mawili ya Unguja pamoja na matumizi sahihi ya fedha za mfuko wa jimbo," alisema.

Katika ziara hiyo alitembelea bonde la mpunga la Cheju na kupewa taarifa za mikakati ya kilimo cha kisasa ambacho kinalenga kuzalisha chakula cha kutosha.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alisema serikali imejipanga kuongeza eneo la kilimo cha mpunga cha umwagiliaji maji mashambani kufikia eka 1,5000 ambazo lengo ni kuifanya Zanzibar kujitosheleza na chakula na kupunguza uagizaji wa bidhaa hiyo nje ya nchi.

"Mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi kufikia mwaka 2020 ni kujitosheleza kwa chakula na kuwekeza zaidi katika kilimo cha mpunga ili kupunguza uagizaji wa bidhaa hiyo nje ya nchi," alisema.



Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Adam Kobelo, akizungumzia uboreshaji wa matibabu Kituo cha Afya Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Jamii yageuka 'kichwa ngumu' kutumia kinga Ukimwi

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA ufuatiliaji na tathmini wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Gharibu Said Gharibu, amesema licha ya kwamba bado kuna maambukizi, lakini bado jamii haijawa na utayari wa kutumia kinga hasa kondomu wakati wa kufanya tendo la ndoa.

Alisema kuwa hali hiyo imejitokeza kutokana na jamii hiyo kuelewa kwamba kutumia njia hiyo wakati wa kujamiiana ni moja ya kuhamasisha zinaa.

Gharib aliyaeleza hayo katika mkutano wa siku moja wa waandishi wa habari wa kuwasilisha mpango mkakati wa wa matumizi ya kinga ulioandaliwa na tume hiyo mjini Zanzibar.

Akiwasilisha ripoti ya utafiti wa mkakati huo mbele ya waandishi wa habari, alisema kuna haja ya kuangalia matumizi ya kondomu hasa kwa makundi maalumu.

"Jamii haitumii kinga ipasavyo ikilinganishwa na makundi maalumu kwa kuhofia kuona kwamba watakuwa wanahamasisha zinaa," alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Habari, Utetezi na Mawasiliano wa tume hiyo, Sihaba Saadati, alisema kuwa mpango huo mkakati umefanyika kwa lengo la kuongeza elimu juu ya kutumia kinga katika makundi tofauti hasa jamii na kuongeza juhudi za kuimarisha matumizi sahihi.

Alisema kuwa mpango huo utatumika kwa mujibu wa mila, desturi, silka na utamaduni wa Mzanzibari kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi na maradhi ya kujamiiana na mimba zisizotarajiwa.

Alieleza kwamba katika kupanga mpango mkakati huo waliangalia kama Zanzibar kuna haja ya kuhamasisha utumiaji wa kinga hiyo ya kondomu na kugunduwa ipo ingawa upatikanaji wake ni mdogo kutokana na matumizi yake kuongezeka kwa asilimia nne ikilinganishwa na miaka 10 iliyopita.

Saadati alisema kuwa katika utafiti uliofanywa mwaka 2016 vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 15 wamekuwa wakifanya ngono pasipo kutumia kinga, huku Wilaya ya Chake Chake Pemba ikiongoza kwa kuwa na asilimia 44 ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini Unguja ambayo ina asilimia 19.

Wakichangia katika mkutano huo waandishi wa habari walisema kuwa kuna haja ya kuongeza elimu zaidi kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya utumiaji wa kondomu ili kupunguza maambukizi ya ukimwi.

# Watakiwa kutumia redio za jamii kufikisha ujumbe

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAOFISA wa habari katika wizara na taasisi za serikali wametakiwa kuzitumia redio jamii ziliopo katika wilaya mbalimbali za Unguja na Pemba kwa ajili ya kutoa taarifa za utekelezaji wa malengo endelevu. Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano Ikulu ya Zanzibar, Hassan Khatib, katika mkutano uliowakutanisha maofisa wa habari kutoka wizara na taasisi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema mchango wa redio za jamii ni mkubwa katika utekelezaji wa malengo endelevu 17 yaliyowekwa na umoja wa mataifa ambayo wananchi wanapaswa kuyafahamu kikamilifu.

Alieleza kwamba utafiti uliofanywa na Ofisi ya Mawasiliano Ikulu umebaini kwamba wananchi bado hawajayafahamu kikamilifu malengo endelevu ya dunia ambayo yanaigusa jamii moja kwa moja.

Khatib alisema kama redio jamii zitatumika kikamilifu kwa ajili ya kutoa taarifa za utekelezaji wa malengo endelevu, ambapo jamii itakuwa katika wakati mzuri wa kufahamu matokeo hayo.

Aidha, Khatib alisema miongoni mwa mikakati ya serikali zote mbili ni kufikisha taarifa za utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020 ambayo mafanikio yake yanatakiwa kufahamika na wananchi. Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua kubwa ya mafanikio, huku sekta ya elimu ikiongoza uandikishaji wa wanafunzi elimu ya maandalizi ambayo sasa imefanywa kuwa ya lazima.

Aliongeza kuwa tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imefuta michango yote iliyokuwa ikitolewa na wazazi, ambapo sasa elimu ya msingi hadi sekondari hakuna michango.

"Yapo mafanikio makubwa katika sekta ya elimu yamefikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwamo kufuta michango ya ada za wanafunzi wa sekondari hatua ambayo imetoa unafuu mkubwa kwa wazazi kuwapunguzia mzigo," aslisema.

Aidha, aliishauri Tume ya Mipango Zanzibar kutoa tafsiri sahihi ya ukuaji wa uchumi kwa wananchi pamoja na kukua kwa pato la taifa ili jamii iweze kufahamu vizuri maana hizo.

"Wananchi wengi unapowaambia uchumi umekuwa na pato la mwananchi mmoja mmoja hawafahamu vizuri na unaonekana kama unafanya viroja kwa sababu tafsiri za maneno ya uchumi hazifahamiki vizuri kwa jamii yetu ya kawaida ikiwamo wananchi waliopo vijijini," aslisema.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo Zanzibar, Dk. Juma Mohamed Salum, alisema vyombo vya habari mchango wake mkubwa katika kufanikisha malengo ya serikali na kazi zake pamoja na sera zinazotekelezwa kwa jamii. Alisema redio jamii zilizopo vijijini bado hazijatumika vizuri katika kutekeleza malengo yake ambayo ni kutoa taarifa zinazoihusu jamii katika sekta mbalimbali.

"Ili redio jamii ziweze kufanya kazi zake vizuri, zinatakiwa zipewe taarifa za matukio mbalimbali ya utekelezaji wa ilani pamoja na malengo endelevu kwa jamii na kufikisha ujumbe huo kwa wananchi walio wengi na kufaidika nao," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MACHI 30, 2019



**RIYAMA AWAKOROMEA VIVURUGE**

Soma UK.15



# UNGA NA NGONO

## Card B abanwa kuwalewesha wanaume

BASI SAWA



# Muumin kufufua Double M yake

MWINJUMA Muumin yuko kwenye mkakati kuhakikisha bendi yake ya Double M Extra inarudi jukwaani tena katika viwango kama ilivyokuwa mwaka 2002.

Ameteja anachokifanya sasa ili kuuweka sawa mkakati huo na kuona kuwa anai kurudisha kundini wanamuziki alioanza nao wakati huo na kuiweka bendi matawi ya juu.

"Kwa muda mrefu nimekuwa na wanamuziki wachanga, lakini sasa nimeanza kuwarudisha mwimbaji Bashir Uhadi, mpiga solo Rashid Sumun na mpiga drums Michale Liloko, ninaendelea kusaka wengine," amesema Muumin.

Amesema licha ya kwamba kwa sasa bado vyuma vimekaza, ana uhakika kufikia katikati ya mwaka huu bendi hiyo itakuwa tayari imeimarika ikiwa na wanamuziki wachanga na wakongwe.



# Voice Wonder bado yupo yupo tu

VOICE Wonder amekwama kurejea kwenye 'gemu' kwa muda aliokuwa amejipangia akidai kwamba ni kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wake.

Amesema alikuwa amepanga kuanza kufanya vitu vyake Januari mwaka huu akiwa na vibao viwili, lakini ameahirisha hadi mwezi ujao, ambapo atatambulisha kibao kimoja tu kiitwacho 'Kitu Kamba'.

"Katika maisha unaweza kupanga jambo lako, lakini Mungu akalibadilisha ndivyo ilivyotokea kwangu, lakini sasa nitarejea rasmi kwenye 'gemu' mwezi ujao nikiwa na 'Kitu Kamba' nilichomshirikisha Barnaba," amesema Wonder.

Amewaomba radhi mashabiki wake waliokuwa wakisubiri ujio wake kwa hamu na kuwataka wamvumilie hadi Aprili atakapoitambulisha 'Kitu Kamba'.



# Shilole awakubali wanaomgeza

MSANII wa filamu, Zuwena Mohamed 'Shilole', amesema anajisikia fahari kwa kuona baadhi ya watu wakiwamo wasanii, wakiiga vitu anavyovianzisha.

Kwa mfano nilianzisha biashara ya kuuza chakula jijini Dar es Salaam, baadaye baadhi ya wasanii nao wakajitokeza kuifanya," amesema Shilole.

Amesema wasanii walikuwa wamebweteka wakitegemea kuigiza tu, lakini yeye Shilole alipoanzisha biashara ya mamalishe, wenzake nao wakamuiga.

"Ninapoona watu wananiiga ninafurahi sana kwa kuwa nami ni mbunifu na sasa anajipanga biashara hiyo hadi mikoani akiwamo kwao Igunga Tabora.

## INSTA-TWITTER





Siku mkisikia nimebadilishana na mtu nikampa gari akanipa sahani yake ya chakula, msishangae. chakula kinabadilika sasa badala ya kuvutia ukile unatamani ukibandike ukutani - **Peter Msechu.**



Tunashukuru sana Taifa Stars maana hatukulala mapema, natamani Baba Keagan angesema tuendeleze nusu bei ila ndio hivyo - **Johari.**



## Luiza Mbutu kama Bi. Kidude

MWIMBAJI wa bendi ya Twanga Pepeta, Luiza Mbutu, amefunguka kwamba kama Mungu ataendelea kumjalia kuwa hai atazeekea katika fani kama ilivyokuwa kwa Bi. Kidude.

"Kwa sasa nina miaka 21 kwenye fani na sitarajii kustaafu kwa sababu kuimba hakuna umri, mbona Bi. Kidude alifariki akiwa bado anaimba? Na mimi nitafanya hivyo iwapo Mungu atanijalia kuwa hai," amesema Mbutu.

Amesema haoni sababu ya kumfanya apumzike muziki haraka wakati kazi ya kuimba siyo ngumu kama unenguaji, ambako unafika wakati viungo vya msanii vinahitaji kupumzika.

UNASEMAAA...

## Mshiko kwanza, kujuana baadaye - Kingwendu

NYOTA wa vichekesho, Kingwendu ametaja vigezo anavyozingatia kabla ya kushirikishwa kwenye video za nyimbo za wasanii, kundi au bendi.

"Kwanza kabisa ni mshiko, ujumbe wa wimbo na pia ninaangalia kama msanii anajulikana au hajulikani, vinginevyo sitaki kushirikishwa," amesema.

Msanii huyo anayetamba na wimbo wa 'Ukerewe' amesema yeye ni kivutio katika video, hivyo hawezi kujishusha thamani ili mwingine afaidike.

Kingwendu amesema muziki ni biashara, hivyo anayemfuata ili kushirikishwa katika video ni lazima awe amejipanga vizuri ili baadaye wasisumbuane.



BODA 2 BODA

## Riyama awakoromea vivuruge



MWIGIZAJI wa filamu nchini Riyama Ally anakerwa na mtindo wa baadhi ya wasanii wa kutafuta umaarufu kwa kufanyiana vurugu.

Amesema msanii ni kioo cha jamii na anatakiwa kutambulika au kupata umaarufu kupitia kazi zake za sanaa anazozifanya na siyo zaidi ya hapo.

"Ninasema hivyo kwa sababu wapo baadhi yao siwataji majina, wanajihusisha na vitendo hivyo wao kwa wao ili kutafuta umaarufu, wanachofanya ni kutojiamini na pia ni ushamba," amesema Riyama.

Amewataka wasidhalilishane wao kwa wao na pia wasiidhalilishe sanaa bali wajitahidi kutengeneza filamu zitakazowapaisha.




@burudanitele


>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Stars,** mwendo ni uleule nikuchapa tu tatu kwenda mbele **-Juma Nature.**



**Nimesikia** mkichamba kuhusu jezi uwanjani sijui nini, mmeshawahi kusikia mi nauza jezi? Mimi nauza nguo za kushona. Insta kuna wachambaji au wasogeza saa mbele kwa wasioangalia TV? Barabara zingine hazina lami, fulu kokoto, fulu kokoto. Kuharibiana mwezi huu mshindwe **- Jacline Wolper.**



**Basi** unaweza ukakuta kuna nchi haijafuzu kwenda AFCON 2019, nashindwa kabisa kuwaelewa, kwa nini? Mnashindwaje yaani? **- Mwana FA.**

# Kuumbe!

# Wasanii Bongo Fleva wapenda soka



**Na Adam Fungamwango**

WASANII wa Bongo Fleva na waigizaji Bongo Movie ni kama binadamu wengine, hivyo nao pia wana mapenzi na mambo, vitu mbalimbali, pamoja na michezo mingine pia mbali na nyanja ya muziki na filamu.

Baadhi waliwahi kucheza michezo mbalimbali ikiwamo soka, huku wengine wakiwa ni wanachama, wapenzi na mashabiki wa timu kubwa na ndogo.

Leo tunafungua mafaili ya wasanii watano wa Bongo Movie ambao mbali na kazi yao ya uingizaji pia ni wanamichezo na ni mashabiki kindakindaki wa soka na wakati mwingi huwa hawakosi uwanjani.

Kumbuka hawa si wale wapenzi wa soka wa kuhamasishwa, bali hawa hata ukienda kwenye mechi za Ligi Kuu utawakuta uwanjani. Ni kitu iko damuni.

**1. Hashim Kambi**



Kwa vijana wa kizazi cha sasa wanamtambua kama ni mwigizaji wa muvi maarufu sana akiwa amecheza filamu nyingi mno.

Lakini, wale wa kizazi cha nyuma kidogo wanamkumbuka Hashim Kambi, kuwa alikuwa mchezaji wa nafasi ya kiungo kwenye klabu ya Yanga, akicheza pamoja na kina Charles Boniface Mkwasa, ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Yanga.

Kijana yeyote anayemwangalia mzee Kambi kwa sasa akiwa tayari ni mtu mzima, ajue kuwa alikuwa mchezaji wa kutumainiwa wa klabu kubwa nchini ya Jangwani miaka ya '80.

Hata hivyo si ndugu na Sahau Kambi. Huyu naye alikuwa mchezaji tegemeo wa Yanga, miaka ya mwisho ya 1980 na 90, akijiunga na Wanajangwani akitokea Reli ya Morogoro. Hayupo kwenye Nyanja za Bongo Movie.

**2. Mboto Haji**

Ni msanii mchekeshaji ambaye aliyejizolea umaarufu mkubwa nchini. Haji hajifichi kabisa kuwa yeye ni shabiki mkubwa wa Yanga.

Amekuwa akivunja watu mbavu kwenye Uwanja wa Taifa au wa Uhuru wakati timu yake ikiwa imepata ushindi.

Kwenye mitandao ya kijamii pia amekuwa akirekodi vituko mbalimbali kwa ajili ya kuisifia timu yake na kuikejeli Simba, ikiwa ni moja ya utani wa mahasimu hao wa jadi.

**3. Jacob Steven JB**




JB ni mmoja wa wasanii wanaopendwa mno na mashabiki wengi wa filamu nchini kutokana na aina yake ya uigizaji, inayochanganyikana na ucheshi na maneno ya hapa na pale.

Huyu ni Simba damu amekuwa hakosi uwanjani pale timu yake inapocheza hasa jijini Dar es Salaam, iwe Taifa au Uhuru.

Wakati mwingine timu yake inapopata ushindi na kufurahi amekuwa akitoa pesa mfukoni na kutunza wachezaji. Hashindwi kuimba singeli 'Naipemba Simba shabiki wa damu.'

**4. Steven Kigosi 'Ray'**



Mmoja wa wasanii nyota nchini ni Steven Kigosi maarufu kama Ray.

Huyu ni mmoja wa mashabiki wakubwa wa klabu ya Yanga. Ray ni mwana Jangwani, hatetereki wala hajifichi kwenye mapenzi yake na klabu ya Yanga, akiwa anaonekana amevaa jezi za timu hiyo uwanjani, lakini pia akitoa maoni mbalimbali juu ya timu yake kabla na baada ya kucheza mechi kwenye runinga.

**5. Mtitu**

Anaitwa William Mtitu. Huyu ni mwigizaji, mwandishi na mwongozaji wa filamu. Pia ni kiongozi wa wasanii wa Bongo Movie.

Ni mwanachama na shabiki wa kutupwa wa Wekundu wa Msimbazi ni mwana Simba hasa. Kutokana na ushabiki wake, alizawadiwa kadi ya uanachama na aliyekuwa wakati huo Rais wa Klabu ya Simba, Evance Aveva, kwenye tamasha la Simba Day mwaka 2015. Kwa sasa ni mwanahisa wa klabu hiyo baada ya kuingia mfumo wa kuuza hisa za timu hiyo.



# DANZAK ATAIWEZA BONGO FLEVA BILA KIKI?



**Na Adam Fungamwango**

NIMEMSIKIA msanii wa muziki wa Bongo Fleva Mtanzania aliyekuwa akiishi nchini Oman, Danzak, ambaye amerejea nchini kwa ajili ya kuuendeleza muziki huo.

Nikamsikia pia Steve Nyerere, ambaye naona ni mmoja wa mameneja wake wakimpigia promo ya nguvu.

Danzak ambaye kwa hapa Bongo anatokea Tanga, si tu kwamba amereja nchini kuendelea na gemu bali amekuja nchini kuubadilisha muziki wa Tanzania.

"Naomba sapoti, tumeamua kuja kufanya muziki nyumbani ili kubadilisha mwendo wa muziki unavyoenda. Kwa sababu imefikia wakati muziki wa Afrika Magharibi unaenda mbali zaidi ya muziki wetu wa hapa, kwa nguvu na sapoti ya jamii tunaweza kuufikisha mbali," alisema.

Ukiwasikiliza wote kwa pamoja utagundua kuwa lengo la Danzak ni kuuinua na kuukomboa muziki wa Bongo Fleva nchini.

Ukisema kuukomboa kitu ni kwamba kimetekwa, au hakipo mikononi mwa mwenye haki nacho.

Bongo Fleva iko wapi na imetekwa na nani? Ni kwamba muziki huu uko mikononi mwa mashabiki ambao wao hawaangalii ubora wala viwango vya muziki au nyimbo, ila wako kwenye ushabiki tu wa kambi fulani. Kundi au upande mmoja hata likitoa ngoma ambayo haina ubora, italazimishwa tu ipendwe na kukubalika na kutafutiwa sifa za uongo. Na ya upande wa pili itapondwa tu, hata kama ni nzuri tena ina ubora.

Hata zamani haikuwa hivyo. Mashabiki wa bendi za Msondo Ngoma na Sikinde pamoja na uhasimu wao, lakini walikuwa wakizikubali baadhi ya tungo za wenzao bila matatizo. Kusifia au kukubali nyimbo za mwenzako hazikufanyi kutokuwa na sifa za kuwa kwenye kambi unayoishabikia.

Kwa sasa pia Bongo kuna baadhi ya mashabiki wanataka nyimbo za ngono na mapenzi tu, za kuonya na mambo mengine ya kijamii hawana mpango nazo kwa madai zinawazingua tu.

Danzak yeye kakaa sana nje, ingawa alianza muziki hapa hapa nchini mwaka 2006 chini ya G Love, akae akijua usanii ule wa zamani sio wa leo.

Wasanii wengi nyimbo za sasa wanatengeneza mashairi ambayo yanakuwa na maneno tata, ya ukakasi masikioni kwa wasikilizaji wenye kujiheshimu.

Ule utata, au maneno yenye matusi japo hayawekwi ndiyo yanayosababisha ngoma zao zipendwe na kukusanya mashabiki lukuki bila kujali hata kama zinapotosha jamii, au zitaleta tafrani na mamlaka za kusimamia nidhamu za wasanii. Wapo wasanii ambao ni lazima wazue taharuki wakati wanapokuwa wanajiandaa kuipua ngoma mpya mfano Mwanza- Nyegezi.

Baadhi ya wasanii hawaamini kama ngoma zao zitatikisa kutokana na mirindimo, maudhui na video bora, bali ni kufanya vituko chochote cha ajabu, hata kama ni kujidhalilisha ili mradi tu awe na kiki kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Huo ndiyo wakati wa kuachia ngoma yake.

Mashabiki wengi wa sasa nao wameshazoea au kuzoeshwa hivyo, nao wanakwenda vivyo hivyo.

Ili kuukomboa muziki wa Bongo Fleva, Danzak atatakiwa aanzie hapo.

Tayari amechia ngoma inaitwa 'Loco'.

Lakini cha kujiuliza anaweza kwenda tofauti na wenzake? Ni muziki wake tu ndiyo utakaomfanya mashabiki kuvutiwa naye na si skendo, vituko au ngoma zenye maneno ya ajabu ajabu? Au na yeye atageukia huko huko kwa wenzake? Tusubiri.

Karibu uboreshe muziki wa Bongo.

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA




1. Matokeo ya 'punguzo la bei' ndio hayo sasa - Mama Nah, Manzese DSM.
2. Walisema wahenga, pombe siyo chai. Unaona sasa mlinzi kalala - Mama Nah, Manzese DSM.
3. Hili joto likiendelea navua mpaka ngozi yangu - Beneali Moussa Beneali, Migombeni Zenji.
4. Si utani, babake alipania sana punguzo la bei la Kwa Mkapa - Elisante Mbunda, Manyoni Singida.
5. Daaah! Huyo lazima atakuwa 'afande' wa walinzi halafu kalewa - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
6. Mambo hayo fanya huko huko Dar, Iringa unapotelea kwenye sufuria - Deo Sanga, Makete Njombe.
7. Babu vipi, viatu vimekuchosha nini? - Adinani Mrutu, Kiwalani DSM.
8. Tatizo la kilevi bila kula nyama - Shirima, Morogoro.
9. Ni pozi tu jamani, wala msinijaribu - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
10. Kwa hili joto la mjini, ngoja nijinafasi kwenye kaupepo - Agatha Mbale, Moro Town.
11. Mbwa huko kijijini, mjini wote watu - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
12. Acha kukoroma na ulevi wako wewe, bisi wako anakuja utafukuzwa kazi - Annah Gumbo, DSM.
13. Mmenilisha biskuti mnashangaa nini nikivaa kama nyinyi? - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
14. Ama kweli mbwa wa mjini wanafaidi, wanavaa mpaka milegezo! - Athanas Gumbo, Mbagala DSM.
15. Leo nimetinga suruali, kesho namalizia koti na tai - Flora, Temeke.
16. Unapoingia Sumbawanga usiwe mjuaji saaana, yatakukuta kama huyu jamaa - Mfaume Mbugi, Mshindo Iringa.
17. Ngoja wezi wanione mlevi, halafu watajua kwa nini nilifanywa kuwa mlinzi - Baby Natasha, Magomeni DSM.
18. Jamani sijalewa, nasumbuliwa na malaria kali - Butelezi Bunyoro, Mwandiga Kigoma.
19. Hapa sasa kausingizi katakuja, koti lilikuwa na joto balaa! - Simon Mvungi, Sinza DSM.
20. Ushauri wa bure. Siku nyingine usifakamie pombe za bure - Mama D., Michenzani Zenji.
21. Naona kibarua chake kinaota nyasi hivi hivi. Sio kwa kulewa na kulala huko - Mahija Jumbe, Ngamiani Tanga.
22. Sio siri, pombe za leo zilikuwa tamu sana tatizo hazikuwa na asusa. Ona nilivyolewa - Mahija Jumbe, Tanga.
23. Ulinzi umenishinda, niache nilale - 0654 865 436.
24. Kwa hili baridi la Iringa, bora nilale kwa kuvae suruali na viatu - Abousalim, Singida.
25. Ulivamia vitumbua ukidhani nyama eeeh! Ona vilivyokulewesha sasa - Mariam Beneali, Migombani Zenji.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Jamani sijalewa, nasumbuliwa na malaria kali - Butelezi Bunyoro, Mwandiga Kigoma.**

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# 'Poor Minds' - Wazazi wanaua mtoto kisa kurithi mali

**Na Adam Fungamwango**

NI heri kukosa mali kuliko kukosa uwezo wakufikiri kwa makini.

Wakati mwingine binadamu anaweza kufanya kitu ukashangaa kama ana akili za kawaida kama wengine au la.

Halafu ukajiuliza kama binadamu wote wana uwezo wa kufikiri sawa, au kila mmoja anafikiri kivyake?

Yapo matukio mengi kwenye jamii ambayo yanaweza kukufanya ukashangaa.

Unaweza kukuta baba, mama au wote kwa pamoja hawataki mtoto wao aoe au kuolewa. Wanataka aendelee kukaa nyumbani muda wote kwao. Ukijiuliza hupati jibu. Wazazi iwe baba au mama anakwenda kupeleka maneno ya fitina kwenye ndoa ya mwanaye ili waachane. Ukijiuliza kwa nini anafanya hivyo hupati jibu.

Filamu ya 'Poor Minds' imelenga kule kule, kuonyesha jinsi baadhi ya wazazi ambao hawaeleweki kama wana roho mbaya, tamaa, kushindwa kufikiri au nini hasa hadi kutokuwa na upendo na watoto wao wa kuwazaa wakiwanyanyasa na wakati mwingine hata kuwaua.

Waliocheza filamu hii ni Yusuph Mlela, Grace Mapunda, Diana Kimaro, Slim Omary, Seif Mbembe na wengineo.

Mbembe na Grace wana watoto wawili ambao ni Mlela na Diana.

Hata hivyo, Mbembe anamtelekeza mkewe na watoto hao na mzigo wa kuwalea unakuwa wa kwake.

Pamoja na kuwalea, lakini pia hana mapenzi na watoto hao, labda kwa vile baba yao aliwatelekeza. Wanaishi kwa taabu, huku Mlela akiwa ndiyo anachukiwa zaidi na mama yake kutokana na kwamba hana kazi na amekuwa akiishi kwa kumtegemea muda wote hadi ukubwani.

Hata hivyo, pamoja na kulelewa kwa shida, watoto wenyewe, Mlela na Diana wanapendana kupindukia.

Hatimaye Mlela anapata kazi na kubadilisha kabisa maisha ya familia yake. Angalau hii inamfanya mama yake Grace kuanza kuwa na mapenzi naye.

Dunia haina siri, baba mzazi mzee Mbembe akasikia kuwa mtoto wake Mlela kwa sasa amepata kazi na ana mapesa kama bilioni, maisha yake ni mazuri yeye na familia yake sasa ni zamu yao kutesa. Anajitokeza na kwenda kuomba radhi kwa mkewe na familia, nayo inamsamehe na kuungana naye.

Wazazi hao wanaonekana wana roho mbaya juu ya mtoto wao.

Baba anamwambia mkewe wamuue kijana wao Mlela ili warithi mali zote alizonazo. Wanakwenda kwa mganga na kutekeleza kile walichoazimia.

Mlela anafariki na kuacha majonzi makubwa kwa dada yake Diana aliyekuwa akimpenda kwa dhati.

Wakati wakiwa na furaha wakifikiria mali zote watarithi wao, madalali wanakuja kwa ajili ya kuwapa notisi ya kupiga mnada nyumba kwa sababu deni halijalipwa kwa muda mrefu.

Wazazi walidhania kuwa nyumba ile ni ya marehemu mtoto wao, kumbe ilikuwa ni ya mkopo.

Pesa ikaanza kukata ndani ya nyumba, Mbembe na mkewe wakaanza kugombana wenyewe kwa wenyewe, hatimaye kulaumiana kwa kumuua mtoto wao.

Ndipo Diana anapogundua kuwa kaka yake kipenzi hakufa kwa ugonjwa, bali aliuawa na wazazi wake.

Anajitokeza na kuanza kuwapa ukweli wao na kuwaambia kuwa hata yeye wanaweza kumuua, hivyo anaondoka kwenda kuanza maisha kivyake. Anawaacha wazazi wake wasijue la kufanya.

# UNGA NA NGONO

## Card B abanwa kuwalewesha wanaume



RAPA aliyejijengea jina nchini Marekani, Cardi B, amejikuta akiwekwa katika kona mbaya ambayo inaweza kumwingiza hatiani kama ikithibitika kuwa ni kweli.

Mwanamuziki huyo ameingia katika sakata zito linalowatafuna mastaa wengi nchini Marekani baada ya kudaiwa kuwalaghai na kisha kuwalewesha wanaume mihadarati kabla ya kufanya nao ngono.

Sakata hilo limeibuka baada ya kuvuja kwa picha ya video iliyozunguka kwa kasi mitandaoni akionekana akisema kuwa aliwalewesha na kuwaibia wanaume waliokuwa wakitaka kujamiana naye wakati alipokuwa akifanya kazi ya kunengua kabla ya kuwa maarufu.

Card B amekosolewa baada ya video hiyo ya Instagram iliyorekodiwa miaka mitatu iliyopita, akieleza namna alivyowanyanyasa wanaume hao na kisha kuwaibia. Mara baada ya kusambaa kumeibuka na kampeni kali maarufu kama #Surviving CardiB, ambayo watu wanafananisha kitendo hicho sawa na kile cha R. Kelly ambaye kwa sasa amefunguliwa kesi ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya wasichana wadogo.

Watu hao wamefika mbali na kuwataka wanaume waliofanyiwa kitendo hicho kujitokeza ili sheria ichukue mkondo wake. Baadhi ya watumiaji wa mitandao ya kijamii wanamfananisha na mchekeshaji Bill Cosby, ambaye alihukumiwa kifungo mwaka 2018 baada ya kushutumiwa kuwalewesha wanawake kwa dawa na kuwadhalilisha kingono.

Baada ya kusambaa kwa video hiyo, Card B, ameamua kujitokeza na kueleza hakufanya kosa kusema hayo.

"Sijawahi kusema kuwa mimi ni msafi sana au natoka ulimwengu ulio mzuri sana." Alisema mwanadada huyo. Awali video hiyo ilirekodiwa wakati ndio ameanza kazi yake na lilikuwa jibu kwa mtu aliyesema kuwa hana haki ya kuwa mwenye mafanikio kwa kuwa hafanyi kazi yoyote.

"Hakuna nilichokua napata. Hakuna," alisema kwenye video hiyo, kabla ya kuweka wazi kuwa alikuwa akiwaalika wanaume kwenye hoteli kabla ya kuwanywesha na kuwaibia," ilisema video hiyo.

Akijibu shutuma hizo, aliandika kwenye ukurasa wa Instagram akieleza kuwa alikuwa akizungumza mambo yaliyopita mazuri au mabaya ambayo yalimsaidia kuishi.

"Mimi ni sehemu ya utamaduni wa hiphop ambapo unaweza kueleza wapi umetoka, na hata mambo mabaya uliyoyafanya kufika ulipo leo." Alisema mshindi huyo wa tuzo za Grammy.

Hata hivyo, alishangaa suala lake kuonekana la ajabu kwa kuwa kuna wanamuziki wengine ambao wanasifu mauaji, vurumai, matumizi ya dawa za kulevya na wizi".

Aliandika: "Sikuwahi kujisifu kwa vitu vilivyojitokeza kwenye video, sikuviweka kwenye muziki kwa sababu sijivunii na ninawajibika kutosifia."

Cardi B alimaliza kwa kueleza wanaume aliowazungumzia kwenye video yake ya zamani kuwa walikuwa wakijua wanachokifanya.

# Lil Wayne hiyo sasa shari



RAPA mwenye utata mwingi, Lil Wayne ametangaza kulihitaji daftari lake lenye orodha ya ngoma zake kadhaa ambalo lilitangazwa kuuzwa kiasi cha shilingi milioni 500 siku kadhaa zilizopita.

Inaelezwa kuwa kijana mwenye daftari hilo ametoa kauli na kusema kuwa Lil Wayne atatakiwa kununua daftari hilo kama watu wengine.

Kwa mujibu wa TMZ imeripotiwa kuwa wakili wa Wayne, ameandika barua ya onyo kwa kampuni ya Moments In Time na kudai kuwa mmiliki wa daftari hilo ana haki na hivyo kijana huyo hana mamlaka ya kukiuza wala kumkabidhi mtu yeyote.



## Fresh Kid rudi shuleni, mama kasema

ACHA! Ndivyo Waziri wa Vijana na Watoto wa Uganda, Florence Nakiwala, amekuja juu akimtaka msanii wa muziki wa rap ambaye ni "Fresh Kid" kuachana na muziki huo na kurejea kwenye masomo.

Patrick Ssenyonjo, mwenye umri wa miaka 7 amekuwa akikosa kuhudhuria masomo shuleni kutokana na kuelemewa na maonyesho ya muziki.

Waziri Nakiwala ameonya mtoto huyo kuanza kuzoeshwa maisha ya kutumia pesa na kuzitafuta akiwa na umri huo mdogo.

## Adesua waambie utamu wa embe anaujua mlaji

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Adesua Etomi, amejibu tuhuma zinazotolewa na watu mbalimbali kutokana na picha yake kupamba jarida maarufu la Vogue.

Baadhi ya watu wametoa maoni yao kuhusu picha hiyo na kueleza inafanana na enzi ya utumwa kutokana mwonekano wake.

Adesua Etomi akijibu maoni hayo amesema anajivunia kuwepo katika jarida hilo na kueleza fursa hiyo ni muhimu kwa nchi ya Nigeria kutokana na kuwa mmoja wa wasanii waliotambuliwa ulimwenguni.





## Jussie mshukuru Mungu kwa wema wake

MWIGIZAJI wa filamu ya Empire, Jussie Smollett, amewashukuru mashabiki wake kwa kuwa karibu naye wakati akikabiliwa na makosa ya kuidanganya polisi katika tukio la kushambuliwa.

Machi mwaka huu msanii huyo alishtakiwa kwa makosa 16 ya kuidanganya polisi na kudaiwa kupanga shambulio la kupigwa na watu wawili wasiojulikana kwa madai ya ubaguzi wa rangi na tuhuma za ushoga.

Inaelezwa kuwa Jussie Smollet alituma barua ya ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa mapenzi ya jinsia moja kwa kampuni ya Fox studio anayofanya nayo kazi siku moja kabla ya shambulio.

## Omotola mbona hueleweki?

MWIGIZAJI nyota wa Nollywood, Omotola Jalade, ameibua mjadala katika mitandao ya kijamii baada ya video yake fupi kuwa na utata.

Nguli huyo wa filamu anayezidi umri wa miaka 40, kwenye video hiyo aliyoitupia Instagram ameonekana akicheza katika mitindo ya mapigano, huku akiwa katika jengo la kizamani.

Omotola ambaye alivaa gauni la mama wa nyumbani amewashangaza wengi kutokana na mwonekano wa nyumba hiyo kukuu ambayo wengi wanajiuliza mazingira hayo ni ya wapi?



SAFU



## Mionzi ya Sheria

# Usidhani mwendo mdogo barabarani ndiyo usalama

Na John Juma
0716217615

HILI madereva mlisikie siyo tu kwa mwendo kasi, hata ukiendesha mwendo pole yote haya yanakupeleka kwenye kulimwa faini barabarani.

Baadhi ya Watanzania wametawaliwa na dhana kuwa kuendesha gari kwa mwendo mdogo ndiyo ustaarabu na ndiyo hatua nzuri inayoelekezwa na sheria zikiwamo za usalama.

Kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Sheria ya Usalama Barabarani, sura namba 168, sheria inakinzana na kuendesha kwa kasi ndogo.

Ndiyo maana kifungu hicho kinaeleza kuwa dereva wa gari ambaye bila sababu za msingi ataendesha kwa mwendo mdogo na kuwasababishia watumiaji wengine wa barabara usumbufu, atakuwa ametenda kosa na panapo hatia, atatakiwa kuadhibiwa kwa kulipa faini.

**UFAFANUZI**

Kifungo cha maneno kinachosomeka' bila sababu za msingi' kina maana kuwa kama itatokea dereva akaendesha kwa mwendo mdogo, mhusika huyo ni lazima awe na sababu za msingi za kufanya hivyo, kinyume na hapo hatakwepa hatia dhidi ya uvunjifu huo wa matakwa ya sheria.

Mahitaji ya kifungu 'sababu za msingi' ni kama vile kuwapo na msongamano mkubwa wa magari (foleni) barabarani, ajali, misafara rasmi, ikiwamo ya viongozi, maandamano na hali inayowalazimu madereva kuendesha magari kwa mwendo mdogo.

Sababu nyingine ni kuwapo na maelekezo ya vibao na alama za usalama barabarani ambavyo vinaweza kuwa na ujumbe kuwa barabara ni mbovu kwa mfano ina makorongo, uchakavu imekatika, daraja bovu yote hayo yakimkwamisha dereva kuendesha kwa mwendo mkubwa.

Suala la ubovu wa gari, wenyewe japokuwa unaweza kuwa moja ya sababu inayosababisha madereva kuendesha na kutembea taratibu, haitoshi kuwa msingi wa utetezi.

Sheria husika inaelekeza gari likiwa bovu lisiingie barabarani kwa namna yoyote kusema kuwa gari lako ndilo linalosababisha kuendesha mwendo huo ni kuvunja sheria. Unatakiwa kuliweka pembeni ili kulirekebisha au kutafuta namna nyingine mbadala.

Kimsingi, lengo kuu hapa ni kuwaepusha watumiaji wengine wa barabara za umma na usumbufu usio na sababu wala umuhimu iwe imefanywa kwa makusudi au kwa namna nyingine.

Kwa hiyo dhana kuwa kuendesha gari kwa mwendo mdogo ndiyo uendeshaji makini na bora zaidi ni ya kujiaminisha wala haiku kisheria.

Askari wa usalama barabarani (kwa mujibu wa sheria) anayo mamlaka ya kumsimamisha na kumtoza faini dereva yeyote kwa kuendesha gari kwa mwendo mdogo bila ya kuwapo kwa sababu za msingi.

Imekuwa ni kawaida kuona misururu ya magari kadhaa ya aina mbalimbali yanayoendeshwa taratibu, na hata watu kudhania huko mbele labda kuna tatizo fulani la kiufundi au ajali.

Kumbe sababu ni dereva mmoja wa gari binafsi au daladala ameamua tu kuendesha kwa mwendo mdogo kwa sababu pengine breki zake ni mbovu.

Inatokea wakati mwingine anapigiwa honi, ghafla anakuwa mbogo kwa kufoka kwa hasira kama vile ndiye anaijua vizuri sheria. Itoshe kusema, kufanya hivyo ni kosa kwa kujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani.

Jambo sahihi ambalo lingefanyika ni kumripoti mhusika kwa askari wa usalama ili kupata msaada stahiki, pengine kwa kumkamatwa na kumwadhibu kama sheria inavyoelekeza.

Cha kuzingatia si kujipangia 'speed' ya kuendeshe ukiwa barabarani vibao pamoja na alama za barabarani ndiyo hasa, mwongozo mkuu wa kiasi cha mwendo anachotakiwa dereva kukizingatia awapo barabarani bila kujali eneo alilopo, wakati wa mvua ni usiku wa manane au alfajiri na mapema. Zingatia maelekezo kwenye vibao vilivyoko barabarani.

Ili uwe na amani hatua ya kwanza ni kuhakikisha, kila dereva wa gari, anafuata "alama elekezi za mwendo" zilizoko barabarani.

Kwa maeneo ambapo hazipo basi haifai kuendesha mwendo wa kasi kubwa wala wa kasi ndogo sana pia. Ni vizuri kutumia mwendo wa wastani, hususan kwa barabara za mitaani ambazo mara nyingi siyo rasmi, kwa usalama zaidi.

Sheria ya Usalama Barabarani inazungumzia madereva wa magari pekee imeacha vyombo vingine vya moto kama bodaboda, bajaji, pikipiki za miguu minne yote hayo ni changamoto inayotakiwa kufanyiwa kazi.

Kwa muda mrefu sasa, mwendo wa kasi pekee ndiyo umekuwa ukipigiwa sana kelele kama vile ni kosa, lakini hata mwendo wa polepole na wenyewe unaweza kumtia hatiani dereva wa gari barabarani iwapo kuna vibao vinvyoelekeza utaratibu wa mwendo .

Ni ukweli usio na ubishi kuwa mwendo mdogo pasipostahili unaweza kumsababishia dereva mwenyewe ajali au ukawasababishia watumiaji wengine ajali.

Nilipokuwa naandika safu hii nilikuwa nawaza kuwa huenda kwa namna moja au nyingine jambo hili linaweza kuonekana kama kichekesho, lakini ukweli ni kwamba Watanzania huishi kwa mazoea.

Waangalie sheria na mienendo na taratibu zinazoongoza sekta au maeneo wanayofanyia kazi, kwa kuwa kwenye suala la mwendo mdogo hivyo ndiyo sheria inavyoelekeza.

Lengo ni kuondoa usumbufu usiokuwa wa lazima kwa watumiaji wengine wa barabara. Tafakari, zingatia.



## Kalamu ya Mwalimu

# Sheria kudhibiti utoro ni kikwazo cha elimu

Reubeni Lumbagala

UTORO ni tatizo kubwa linaloripotiwa katika shule nyingi za msingi na sekondari nchini. Ni kikwazo kinachokwamisha maendeleo ya wanafunzi kitaaluma. Mwanafunzi anaposhindwa kuhudhuria shule bila taarifa kutoka kwa mzazi au mlezi wake, huhesabika kuwa ni mtoro na anastahili kuadhibiwa kwa kuwa utoro ni kosa kwa mujibu wa kanuni na sheria zinazoongoza shule.

Ili mwanafunzi aweze kufaulu kikamilifu masomo yake, anapaswa kuhudhuria masomo kila siku bila kukosa ili aweze kupata maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali kutoka kwa walimu wake wenye wajibu wa kufanya hivyo. Kukosekana shuleni kwa mwanafunzi hata siku moja kunaweza kumletea matatizo kutokana na kupitwa na vitu vingi vitakavyofundishwa akiwa hayupo darasani.

Hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kufika shule ili kuhakikisha hapitwi na yale ambayo yanafundishwa.

Kwa kuwa utoro ni kikwazo katika maendeleo ya taaluma, ipo mikakati mbalimbali iliyowekwa na uongozi wa shule husika, kamati na bodi za shule, uongozi wa idara za elimu wilaya, mkoa hadi wizarani kukabiliana na tatizo la utoro. Pamoja na mbinu shirikishi ambazo zinatumika katika kumaliza tatizo la utoro shuleni, ipo haja kwa serikali kuifanyia marekebisho makubwa Sheria ya Elimu Namba 25 ya Mwaka 1978, ambayo inatoa mwanya kwa na wanafunzi watoro ambao wanashindwa kufukuzwa shule kwa muda mwafaka.

Kwa mujibu wa sheria hii, mwanafunzi anapaswa kufukuzwa shule kwa utoro pale tu atakaposhindwa kuhudhuria shule kwa muda wa siku 90 mfululizo ambayo ni miezi mitatu. Sheria hii ni kikwazo kikubwa katika kukabiliana na utoro wa wanafunzi. Kwanza inatoa mwanya kwa wanafunzi kuwa watoro bila hofu na kuhakikisha kuwa wanaepuka kufukuzwa shule kwa kutumia kipengele cha sheria hiyo.

Tafsiri ya siku 90 mfululizo ni kumaanisha kuwa endapo mwanafunzi atashindwa kuhudhuria shuleni kwa siku 89 na siku ya 90 akafika shule, atakuwa na sifa ya kuendelea na masomo kwan kuwa siku ya 90 aliyofika shule itakuwa imefuta utoro wake wote wa siku 89 alizokosa kuingia darasani, hivyo ana sifa zote za kuendelea na shule.

Ifahamike kuwa, sheria hii ya mwaka 1978 ni ya zamani sana na haiwezi kuendana na dunia ya sasa na mambo yaliyopo.

**KIKWAZO KISHERIA**

Nikirejea kwenye sheria hii nashauri mwanafunzi ambaye atashindwa kufika shuleni ndani ya siku 30 mfululizo bila taarifa, afukuzwe shule badala ya kusibiri hadi zifike siku 90 kama ilivyo sasa.

Hii itasaidia kuweka nidhamu kwa wanafunzi katika suala zima la kuhudhuria masomo na kuinua ufaulu wa wanafunzi. Serikali na wadau tafakarini suala hili na kuchukua hatua.

Ikumbukwe, katika dunia hii ya ushindani wa kila kitu ikiwamo elimu, serikali haipaswi kuendelea kutumia sheria ambayo ni kikwazo cha kufikia maendeleo ya nchi kwa sekta ya elimu. Ifike wakati suala la kusoma lisiwe la kubembelezana mwanafunzi, mzazi au mlezi lifanywe na wale tu walio tayari kusoma ili kufikia maendeleo halisi ya kiuchumi na kitaaluma.

Kwa kuwa maendelo haya yanahitaji wahitimu walioandaliwa vyema katika taasisi mbalimbali za elimu, ni vyema wahitimu wakawa wale waliohudhuria kikamilifu shuleni na vyuoni na kuweza kupokea vyote vilivyofundishwa na walimu kwa ufasaha.

Kwa kukosa kuhudhuria shule kwa muda mrefu, mwanafunzi anapitwa na vingi na kusababisha kuwa mhitimu mwenye maarifa yasiyotosheleza.

Serikali inafanya juhudi kubwa za kuboresha sekta ya elimu kwa kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira bora. Juhudi hizi ni lazima ziungwe mkono na wazazi na wanafunzi wenyewe kwa kuhakikisha wanahudhuria masomo bila kukosa.

Na pale ambapo mwanafunzi atashindwa kufika shule kwa sababu za msingi kama kuumwa, kufiwa, ni muhimu taarifa hizo zikafika shuleni ili mwalimu wa darasa aweze kumjazia mwanafunzi taarifa hizo kwenye daftari la mahudhurio ya wanafunzi.

Ikumbukwe kuwa mwanafunzi kutokufika shule kwa muda mrefu bila sababu za msingi na kuhesabika kuwa mtoro sugu, ni kurudisha nyuma juhudi za kukuza sekta ya elimu. Na mwanafunzi wa aina hii anastahili kupata adhabu ya kufukuzwa shule.

Kupitia Sera ya Elimu Msingi bila Malipo, zaidi ya shilingi bilioni 24 zinatumika kila mwezi kugharamia uendeshaji wa elimu katika shule za msingi na sekondari. Hivyo basi ni wakati wa serikali kuwagharamia wanafunzi ambao wana moyo wa kusoma ambao si watoro.

Wazazi na walezi nao wahakikishe wanawasimamia watoto wao ipasavyo, ili waweze kufika shuleni kila siku bila kukosa. Na pale panapotokea sababu za msingi za mwanafunzi kushindwa kuhudhuria masomo, mzazi afike shule kutoa taarifa.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni : (+255) 764 666349.**

# DK. KIHAMIA:

# Mchango wa shule binafsi ni wa kujivunia

Na Mwandishi Wetu

SEKTA binafsi ni mbia muhimu wa serikali katika jitihada za kukuza na kuboresha elimu hapa nchini, hivyo shule binafsi zimekuwa zikijitahidi kuhakikisha zinaweka mazingira bora ya kufaulisha wanafunzi wake wengi.

Kutokana na kutambua mchango mkubwa wa shule binafsi nchini, hivi karibuni serikali kupitia kwa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Athumani Kihamia, ilipongeza uwekezaji unaofanywa na shule binafsi.

Akizungumza kwenye mahafali ya 10 kidato cha sita ya Shule ya Sekondari ya Tusiime, Kihamia, alisema mchango wa shule binafsi ni muhimu kwa kuwa unaunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ambayo imedhamiria kutoa elimu bora kwa kila Mtanzania.

Alisema serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi mahiri wa Rais John Magufuli imedhamiria kuhakikisha vijana wanapata elimu bora kwa manufaa yao na kwa taifa kwa ujumla.

"Tunahitaji vijana wazalendo na wasomi watakaokuwa msaada kwa taifa na watakaosimamia rasilimali za nchi, hivyo maboresho ambayo Tusiime mnayafanya naamini mnaouwezo wa kuendelea kuifanya kuwa sekondari ya mfano kitaaluma," alisema.

Alisema serikali imeweka mikakati mikubwa ya elimu kwa kuwa bila elimu nchi haiwezi kufikia uchumi wa viwanda kama ambavyo serikali ina maono ya kuivusha nchi kuwa na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Wakati huo huo, wahitimu wa kidato cha sita wa shule hiyo waliiomba serikali kuitangaza shule yao kuwa ya vipaji maalum kutokana na mafanikio inayoyapata kitaaluma mwaka hadi mwaka kwenye matokeo ya kitaifa.

Aliyetoa ombi hilo ni wanafunzi Keziah Nyirenda aliyekuwa akitoa hotuba ya wanafunzi wa kidato cha sita mbele ya Mkurugenzi huyo wa (NEC), Dk. Kihamia.

Mwanafunzi huyo alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma mwaka hadi mwaka, jambo ambalo alisema linaweza kuthibitika kupitia matokeo ya mitihani ya ndani ya shule, mitihani ya kanda na ile ya kitaifa.

"Ufaulu huu unatufanya kujivunia kuwa sehemu ya Tusiime na ni ukweli usiofichika kwamba shue yetu ni ya vipaji maalum tunaomba ijulikane hivyo," alisema na kuongeza.

"Mnaweza msituelewe lakini sisi wahitimu pamoja na wazazi ni mashahidi kwa kuwa baadhi yetu Tusiime haikuwa chaguo la kwanza ila baada ya kukosa nafasi shule zingine kutokana na kutokuwa na vigezo vyao, lakini Tusiime ilitupokea kama tulivyo," alisema.



Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Athumani Kihamia, akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari ya Tusiime ya jijini Dar es Salaam, wakati wa mahafali ya 10 ya shule hiyo hivi karibuni. Kulia ni Mkuu wa shule hiyo, Emil Rugambwa na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Dk. John Mbogoma.

Anasema cha ajabu kila matokeo yanapotoka mara zote wamekuwa wakilinganishwa na shule hizo wakati walikuwa wanaonekana hawana sifa ya kuwa katika shule bora.

"Kwa hali hii kwanini shule yetu isiwe miongoni mwa shule zenye vipaji maalum kwani tukilinganisha vigezo vya udahili tunajikuta kuwa shule yetu ni zaidi ya hizo shule...waswahili wanasema usilolijua ni sawa na usiku wa giza, sisi wahitimu tunajuana na ukitaka kujua ubora wa Tusiime tuulize sisi au wazazi wetu," alisema. Mkuu wa shule hiyo, Emil Rugambwa, alisema shule hiyo huwa haichagui wanafunzi wa vipaji maalum kama shule zingine bali huchukua wanafunzi wa aina zote na kuwaandaa vyema kwenye mitihani.

"Wazazi wakati mwingine wanatuletea wanafunzi baada ya kukosa nafasi kwenye shule zingine, lakini sisi na timu yetu mahiri tunawaandaa mpaka wanakuwa bora kwenye matokeo ya kitaifa," anasema Rugambwa.

Alisema shule inatambua mchango wa wazazi wa hali na mali ambao wamewekeza kwa vijana wao kwani haikuwa kazi rahisi sana na aliwapongeza walimu na wafanyakazi wengine wasio walimu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kuwa vijana wanapata kile kinachostahili.

"Natambua kuwa kazi wanayoifanya ni kubwa na wakati mwingine huwezi kuilipa kwa fedha. Wamekuwa wakijituma usiku na mchana katika kuhakikisha vijana wetu wanapata elimu bora kwa mustakabali wa maisha yao, lakini pia hii inadhihirisha upendo mkubwa walionao kwa watoto wetu," anasema Rugambwa.

Anasema shule za Tusiime zimekuwa zikifanya vizuri sana tangu kuanzishwa kwake na ni shule ambayo ina wanafunzi wa hali zote kitaaluma.

"Ni shule ambayo kwa kiasi kikubwa inapata wanafunzi wa kawaida kitaaluma. Lakini tunachojivunia ni kwamba mara zote tumekuwa tukijitahidi sana kwa uwezo na maarifa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia ili kuwaandaa wanafunzi hao kuonekana bora kitaaluma tofauti na matarajio ya wengi," anasema.

"Katika jambo hili wazazi wenzangu watakuwa mashahidi, kwa kuwa ninaimani inawezekana walio wengi Tusiime haikuwa chaguo lao

la kwanza, wameifikiria Tusiime baada ya vijana wetu kukosa nafasi katika shule ambazo walizipa kipao mbele na wengine wameifikiria Tusiime baada ya vijana wetu kupoteza dira huko walikokuwa na kama si

kuonekana kuwa hawastahili tena kuwa katika shule hizo kutokana na maendeleo yasiyoridhisha kitaaluma," anasema.

Rugambwa anasema pamoja na haya yote mara zote wamepambana kufa na kupona ili kuhakikisha wanafunzi wao wanafundishwa na kulelewa katikamisingi inayofaa pasipo kujali tofauti zao ili mwisho wa siku kila mwanafunzi aweze kutimiza ndoto zake.

Anasema baadhi ya wazazi ni mashahidi kwani wanajua mazingira ambayo wamemkabidhi vijana wao ni mazingira magumu.

"Hata hivyo nashukuru Mungu kwa kuwa kupitia timu ya walimu mahiri niliyonayo mara zote tumekuwa tukifanya vizuri, hali inayosababisha kushindanishwa na shule zinazochukua wanafunzi wenye vipaji maalumu. Shule yetu imekuwa ikipanga na kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha miundombinu na mazingira mbalimbali kwa lengo la kuzidi kutengeneza mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia.

Hali hii inatufanya tuweze kwenda sambamba na mikakati inayofanywa na serikali yetu katika kuboresha sekta ya elimu kwa kudumisha na kuboresha miundombinu kwa lengo la kuinua kiwango na ubora wa elimu nchini," anasema Rugambwa.

Rugambwa anasema Tusiime itatahakikisha inaunga mkono serikali ya awamu ya tano kila wakati kwa kuhakikisha inatoa elimu bora inayozingatia mazingira kwa kufuata taratibu na miongozo inayotolewa na serikali kupitia Wizara ya Elimu.

Rugambwa aliwataka wazazi kabla ya kufikiria sehemu nyingine, wafikirie Tusiime kwanza, ambayo imewapa watoto wao malezi na elimu bora kama wanaohitimu huku akisema kuwa shule ni nyingi sana, lakini zinatofautiana sana.

Aliwaasa pia wanafunzi hao wasikubali kudanganywa kwa namna yoyote na kuwafanya kupuuza yale waliyofundishwa na kuanza kuhangaika na uvumi wa mitihani mtaani au kufanya udanganyifu kwa namna yoyote ile kwani wao wana uhakika na walichowapa.

## MAAJABU YA TEKNOLOJIA

# Kompyuta kufikiri kama binadamu-2

**Na Gaudensia Mngumi**

Hii ni sehemu ya mwisho ya makala iliyoanza wiki iliyopita ikielezea maajabu ya teknolojia ya Artificial Intelligence (AI) ambayo ni jitihada za wanasayansi wa kompyuta kuifanya kompyuta iweze kujifunza kama binadamu.

Mbobezi wa kompyuta na mhadhiri katika Idara ya Mifumo ya Kompyuta na Hisabati ya Chuo cha Ardhi, jijini Dar es Salaam, Dk. Katule Ntwa (pichani), anamalizia sehemu ya mahojiano na Nipashe kuhusu utaalamu huo mpya wa kuifanya 'kompyuta kuwaza na kuchemsha bongo kama binadamu, akielezea chimbuko la dhana hiyo.

Anasema kompyuta inalinganishwa na binadamu na kwamba kabla ya kuingia kwenye AI ni vyema kurejea kwenye akili za kawaida za binadamu.

"Binadamu anapozaliwa hakuna anachofahamu. Lakini kutokana na mazingira anayokulia anaanza kujifunza vitu mbalimbali. Cha kwanza ni jinsi ya kuwasiliana. Kwa hiyo atajifunza lugha ambayo wanajamii wanaomzunguka huitumia." Anaeleza.

Pia atajifunza jinsi ya kutambua watu na vitu, mfano anapoiona meza au kiti kwa mara ya kwanza tangu kuzaliwa anaweza asijue ni kitu gani, anaongeza.

Kiasi anavyokuwa, atajifunza kujua ni kitu gani kupitia jamii inayomzunguka, watu watamwambia inaitwa meza au kiti na kazi zake ni zipi.

Kwa hiyo binadamu hujifunza mambo mbali mbali ni kwa mtindo huo, hata wakienda shule ndivyo wanavyojifunza vitu mbali mbali. Vivyo, ndivyo zilivyo juhudi za kompyuta kufundishwa iweze kujifunza kama walivyo binadamu.

Sasa AI ni juhudi za wanasayansi wa kompyuta kuifanya kompyuta iweze kufundishika kama binadamu wanavyojifunza kuanzia utotoni na hata wanapokutana na mambo mapya, anaeleza.

Anasema ili mashine hiyo ifanye kazi kwa kawaida lazima iwekee 'programs' lakini njia hii haifunzi kompyuta bali inaiwekea maelezo ya nini cha kufanya.

"Kwenye AI badala ya kuipa kompyuta maelezo ya nini cha kufanya, tunaipa kompyuta mifano ya kitu fulani halafu kupitia hiyo mifano, inapata maarifa ya jinsi ya kufanya kitu fulani. Kwa hiyo baadaye ikikutana na mfano ambao haijawahi kufundishwa au kuonyeshwa bado inaweza ikautumia ujuzi iliyonayo kutambua kwamba kuna jambo fulani." Anaongeza.

### BIASHARA MITANDAONI

Zama hizi AI inatumiwa kwenye biashara mitandaoni, anasema Dk. Ntwa.

"Ukitembelea maduka ya kuuza vitu mitandaoni, utaona wana pendekeza bidhaa ambazo utazipenda. Je, huwa wanafanyeje? Wanachofanya ni kwamba ukiingia kwenye ule mtandao wanaangalia wapi 'umeclick' wanakusanya taarifa zako za kila unapotembelea kwenye mtandao wao," anasema.

Anaongeza: "Wanajaribu kulinganisha na watu wengine ambao wana mtiririko kama wako ambao walitembelea mtandaoni kabla yako na kuangalia vitu gani vya ziada ambavyo walivichagua ambavyo wewe bado hujavitembelea, kisha wanapendekeza vitu vingine utakavyopendezewa navyo."

Mtaalamu huyu wa kompyuta anasema, kama hutapendezwa na hata pendekezo moja, kompyuta inaendelea kujifunza kutoka kwako kitaalamu ni 'online learning' kwamba inaendelea kujifunza zaidi kwa jinsi inavyokutana na wateja.



Dk. Katule Ntwa



Balozi wa India nchini Sandeep Arya, Ubalozi wa nchi hiyo ndio unaoratibu mafunzo ya sayansi na teknolojia pamoja na fani nyingine kupitia program za ITEC.

### KUMSOMA MTUMIAJI

Dk. Ntwa anasema, aidha, AI inatumika hata katika kupendekeza maudhui ambayo watumiaji wa kompyuta wanapendelea kwenye mtandao.

Kupitia utaalamu huo, inaangalia mwenendo wa mtumiaji na kugundua anapenda nini.

"Nina uhakika utakuwa umeshaona jinsi kwenye 'youtube' muziki na picha unazozipenda zilivyowezesha kompyuta kupendekeza video na vitu unavyovipenda na kila baada ya kusoma tabia zako inapendekeza yale unayotaka," anasema na kufafanua kuwa hiyo ndiyo artificial intelligence.

Anaeleza zaidi kuwa AI ni muhimu kwa kuwa inawezesha kutumia data katika kufanya maamuzi mengi, kwa mfano mataifa yaliyoendelea teknolojia kama 'Google, Youtube, Facebook, Instagram, Spotify au hata Self-driving cars zote zinatumia AI.

Kwa Tanzania maeneo ambapo AI inaweza kutumika kwa sasa ni kama sekta za huduma za jamii kama afya na elimu.

Kwa kutumia AI watendaji na wapanga mipango na hata watu sera serikalini wanaweza kupata taarifa sahihi tena kwa wakati sahihi, kwa kutumia data mbalimbali zilizopo.

"Na pia tunaweza kuona kama kuna mapengo au upungufu 'gap' kwenye sera zetu ili kuandaa mipango ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ziwe za kiafya na kiuchumi."

Mtaalamu huyu anaongeza kuwa kwa upande mwingine teknolojia hiyo inaweza kutumiwa kwenye uanzishaji wa mambo yanayohusiana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Tehama-IT, wataalamu wanaweza kutumia AI kutatua changamoto mbalimbali za kwenye jamii.

Kadhalika inaweza kutumika kujua mahitaji au maoni ya wateja kwenye sekta mbalimbali mfano kampuni za simu na benki, waka kutumia kurasa zao kwenye mitandao ya kijamii, (social media pages.)

Inawezekana kwa sababu mitandao hiyo ina maoni mengi sana ya watumiaji na wateja, hivyo kupitia AI wanaweza kuyachota na kujifunza vitu vingi kuhusu wateja wao, mfano nini wanachopendelea katika huduma, kitu gani hawapendelei, nini wanatamani kiongezeka kwenye huduma zinazotolewa.

Anasema japo data au taarifa zao zipo katika mfumo wa maandishi 'text', lakini kupitia AI zinachakatwa ziwe kwenye mfumo ambao unawezesha mashine kujifunza na kutoa majawabu mbalimbali katika kuboresha huduma.

### AI TANZANIA

Dk. Ntwa, aliyesoma kozi hiyo katika Chuo cha IIT Kanpur huko India anapoulizwa kuhusu mwamko wa teknolojia hiyo nchini, anasema taifa limeanza kuwa na wasomi wengi wa fani hiyo, kwa mfano wapo kutoka maeneo mengi mfano vyuo vikuu, wizarani, mashirika ya umma kama Bima (NIC).

Anasema suala la AI ni la dunia nzima, ndiyo maana mwamko umeongezeka na kwamba umechochewa na teknolojia iitwayo "Deep Learning" ambayo hapo awali ilishindikana kutumika kwa sababu kompyuta zilikuwa na kasi au spidi ndogo.

Kwa sasa zimepata uwezo maradufu wa kuweza kutumia 'deep learning' na hii ikafanya watu wengi waanze kuwa na shauku ya kujua AI.

Anasema hivi karibuni vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Dodoma (UDOM) vimeanza kutoa mafunzo ya uzamili katika Data Science ambayo inahusiana na AI kwenye upande wa Machine Learning. Wakati Chuo cha Ardhi pia kinategemea kuanzisha programu ya uzamili Data Science.

"Pia mwamko umeanza kuwa mkubwa, miaka ijayo tutakuwa na wataalamu wengi zadi. Wapo wanafanya shahada za uzamivu katika eneo hilo kwenye vyuo vya nje na ni walimu wa vyuo mbalimbali nchini. Kwa hiyo AI ni kitu ambacho kinategemewa kupewa msukumo zaidi kwenye mtaala wa shahada ya kwanza ya sayansi ya kompyuta au uhandisi wa kompyuta katika vyuo mbalimbali hapa Tanzania," anasema Dk. Ntwa.

Na Mary Geofrey



Wadau wa Wizara ya Afya wakishiriki mkutano wa uzinduzi wa jukwaa la mawasiliano la Naweza mkoani Iringa hivi karibuni. Mpango huo unalenga kuleta mabadiliko chanya ya tabia kwa jamii. PICHA: MARY GEOFFREY.

# 'Ni mwisho vifo watoto wachanga'

KILA mwanamke mjamzito ana njozi na matamanio ya aina moja ya kujifungua salama na kumuona mwanawe aliye tumboni. Hiyo ndiyo sala, ni fikra za kila wakati na kwa miezi tisa ndicho anachoomba kwa Mungu.

Lakini, wakati mwingine sivyo watoto licha ya kuzaliwa hai hawafikishi miaka mitano, wanafariki. Jambo hili linaumiza kila mmoja, si mzazi pekee hata serikali.

Juhudi nyingi zimefanyika kuokoa maisha yao na sasa Wizara ya Afya na wadau wengine wanaeleza kuwa vifo vimepungua.

Taarifa zinaonyesha kuwa kati ya kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai, wanaofariki dunia ni 57, kwa mujibu wa taarifa za mwaka 2016.

Kwa mujibu wa ripoti zilizotolewa na Benki ya Dunia (WB) hivi karibuni, inaonyesha kuwa kuna mafanikio makubwa katika kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Ripoti hiyo inaonyesha kupungua kwa idadi ya vifo kutoka 179 kati ya kila watoto 1,000 mwaka 1990 hadi kufikia watoto 132 mwaka 2000 na sasa watoto 72 mwaka 2010 hadi watoto 57 mwaka 2016.

Kadhalika, ripoti ya Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), inaonyesha kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano mfululizo.

Aidha, ripoti hiyo inaonyesha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa idadi ya vifo kutoka watoto 166 kati ya watoto 1,000 mwaka 1990 hadi kufikia vifo vya watoto 112 mwaka 2005 na vifo vya watoto 67 mwaka 2015.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Wizara ya Afya kuhusu takwimu za vifo vya watoto, mwaka 2015 idadi ya watoto wachanga 25 hufariki kwa kila vizazi hai 1,000 kila mwaka.

Februari 28, mwaka jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phillip Mpango, akizundua ripoti ya makadirio ya watu nchini, alisema inaonyesha ongezeko la watu limefika milioni 54.2, huku ikikadiriwa idadi ya watu nchini itafika takribani milioni 77.5 ifikapo mwaka 2030.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa pamoja na sababu nyingine, uwepo wa idadi kubwa ya vizazi inayofikia milioni mbili ikilinganishwa na idadi ndogo ya vifo inayotajwa kufikia 400,000 kwa mwaka.

Sababu nyingine ni kupungua kwa vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano.

### VIFO VYA WAZAZI

Licha ya vifo vya watoto wachanga wenye umri chini ya miaka mitano kupungua, bado kuna changamoto ya vifo vya kinamama vinavyochangiwa zaidi na changamoto za umbali wa vituo vya kutoa huduma za uzazi, watalaamu wa kuwahudumia na kukosa au kuwa na elimu ndogo ya afya ya uzazi.

Kutokana na kuwapo kwa changamoto, serikali inaendesha mradi wa Naweza ambao unatekelezwa katika mikoa yote chini ya Wizara ya Afya, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, kimeanza kutoa elimu ya kuhamasisha umma kuokoa maisha na kupunguza vifo hivyo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Wizara ya Afya, vifo vitokanavyo na uzazi nchini ni vingi na kwamba mwaka 2015/16 wanawake 556 kwa kila vizazi hai 100,000 walipoteza maisha kila mwaka.

Hii ni sawa na wanawake 11,000 kwa mwaka na wanawake 916 kwa mwezi au kinamama 211 kila wiki, au 30 kwa siku na takribani mwanamke mmoja kila baada ya saa moja.

Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma katika Wizara ya Afya, Amma Kasangala, anasema kwa kila wazazi 100,000 hii ndiyo idadi ya waliopoteza maisha mwaka 1990 vilikuwa vifo 870, mwaka 2005 vilikuwa 578, mwaka 2010 vifo 454, mwaka 2012 vifo 432 na mwaka 2016 vifo 566 kwa kila vizazi hai 100,000.

Kasangala anataja sababu ya vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga kuwa ni, maambukizi ya VVU, kifua kikuu (TB) na malaria mambo ambayo bado ni tatizo nchini.

Anasema kwa kutambua umuhimu huo, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) pamoja na Mradi wa Shirika la Marekani (USAID) Tulonge Afya, imeandaa Jukwaa la Mawasiliano ya Afya kwa watu wazima na vijana ili kutoa elimu kwa jamii.

"Jukwaa hili ni mkakati wa pamoja unaolenga kutumia mbinu mbalimbali za kushirikisha jamii na kuielimisha kwa lengo la kubadili tabia ili kuboresha afya zao," anasema Kasangala.

Anasema jukwaa la watu wazima linalenga watu wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45 na jukwaa la vijana ni kwa wenye umri wa miaka 15 hadi 24.

Anasema majukumu ya jukwaa hilo yatatekelezwa kwenye afua za malaria, TB, mama na mtoto, huduma za afya ya uzazi kabla na baada ya ujauzito, VVU na Ukimwi.

### SABABU ZA VIFO

Ofisa wa Wizara ya Afya, Programu ya Uzazi Salama, Martha Shakinyau, anasema vifo vingi vya uzazi vinatokana na mwanamke kutokwa na damu nyingi kabla, wakati wa kujifungua au baada ya kujifungua na kwamba asilimia 28 ya vifo vyote huchangiwa na tatizo hilo.

Anasema pia wapo wanawake ambao wanapoteza maisha kwa asilimia 17 kutokana na kupata kifafa cha mimba.

Anasema pia yapo matatizo yatokanayo na kuharibika mimba kwa njia mbalimbali ambayo husababisha vifo kwa kinamama kwa asilimia 19.

Shikanyau anataja matatizo mengine yanayosababisha vifo hivyo kuwa ni uchungu pingamizi kwa asilimia 11 na maambukizi mengine kwa asilimia 11. Anasema magonjwa mengine kama kupungukiwa dawa, maambukizi ya VVU na malaria husababisha vifo kwa kinamama kwa asilimia 14.

"Katika kukabiliana na changamoto hii ndiyo sababu tumeanzisha Jukwaa la Naweza ili kutoa elimu kwa jamii kila mtu kutimiza wajibu wake," anaeleza Shikanyau.

Anasema vifo vitokanavyo na uzazi kwa wajawazito na watoto wachanga vinasababishwa na sababu mbalimbali ikiwamo umbali wa vituo vya huduma za afya, hali duni ya maisha na mila na desturi potofu.

"Zote hizi zinaweza kuzuilika kwa juhudi zinazofanywa na serikali za kujenga vituo vya afya kila kijiji, lakini pia kuweka vifaa tiba na watumishi wa kutoa kwenye vituo vya afya. Jamii nayo inapaswa kushiriki kupunguza vifo hivyo kwa kupata elimu kama hii tunayotoa na kuwa tayari ili kuwahi kwenye vituo vya afya wajawazito wanapoona dalili za hatari kwa mama na mtoto," anasema Shikanyau.

### VIFO VYA WATOTO

Vifo vya watoto wachanga vinasababishwa na tatizo la kushindwa kupumua, kwa asilimia 31 anasema Shekanyau.

Anasema pia matatizo yanayotokana na mtoto kuzaliwa na uzito pungufu huchangia vifo kwa asilimia 25, uambukizo kwa watoto wachanga kwa asilimia 20.

Kwenye huduma, anataja upungufu wa dawa, vifaa tiba na uhaba wa watoa huduma wenye ujuzi. Aidha, huduma hafifu za rufani, ushirikishwaji mdogo wa wanaume na jamii, viongozi wa siasa, viongozi wa serikali, viongozi wa dini katika mambo yanayohusu uzazi salama na upungufu wa damu salama ni chanzo.

### MKAKATI WA SERIKALI

Kupitia kampeni ya "Jiongeze Tuwavushe Salama" iliyozinduliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Novemba mwaka jana jijini Dodoma, serikali imelenga kuhamasisha jamii kuchukua hatua.

Anasema kauli mbiu ni kuongeza kasi ya uwajibikaji ngazi zote za utoaji wa huduma katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga na vifo vya watoto chini ya miaka mitano.

"Katika kutambulisha project ya "Naweza" tunategemea kila mmoja wetu analojukumu la kuikumbusha jamii kuwa kwa pamoja tunaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga na kufikia Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati bila vifo vya makundi hayo," anasema.

Lengo la serikali ni kupunguza vifo vya uzazi kutoka 556 hadi 292 kati ya vizazi hai 100,000 na kwa watoto ni kuvipunguza kutoka vifo 25 kati watoto hai 1,000 hadi 16 kwa watoto hai 1,000 mwaka kesho.

HABARI KIMATAIFA

## Watatu wauawa kwa uasi Comoro

**MORONI,** Comoro

SERIKALI ya Comoro imethibitisha kuwa vikosi vya usalama vimewaua karibu washambuliaji watatu katika tukio la ufyatulianaji risasi lililotokea katika kambi ya jeshi ya mji mkuu, Moroni juzi.

Mkasa huo ulitokea baada ya wanajeshi waasi kuvunja gereza na kutoroka na upinzani ukatangaza mpango wa kumuondoa rais madarakani.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Mohamed Daoudou, alisema kundi la wanajeshi waasi waliofungwa kwa kupanga njama ya mapinduzi mwaka jana walitoroka jela jana asubuhi na kwenda kwenye kambi ya jeshi na kuwashawishi wanajeshi wengine kujiunga nao.

Kiongozi wao, Meja Fayssoil Abdoussalam, ni miongoni mwa waliouawa katika tukio hilo. Milio ya risasi ilirindima katika kambi ya jeshi saa chache baada ya wagombea wa urais wa upande wa upinzani kutangaza mpango wao wa kumuondoa madarakani Rais Azali Assoumani.

Assoumani alichaguliwa tena mapema wiki hii katika uchaguzi unaopingwa na wapinzani kwa madai kuwa ulikumbwa na udanganyifu mwingi. **DW**

## Upasuaji huua wanawake 300,000

**LONDON,** Uingereza

UTAFITI umebaini kuwa wanawake 300,000 kote duniani, idadi kubwa zaidi ikiwa ni raia wa nchi zinazoendelea hufa kila mwaka kutokana na matatizo yanayoibuka kwenye matibabu ya upasuaji.

Utafiti, uliongozwa na Chuo cha Queen Mary jijini London, unaaminika kuwa wa kina zaidi kuhusu suala hilo kuliko utafiti mwingine uliowahi kufanyika.

Watafiti walichambua data za wanawake wajawazito milioni 12 na kukagundulika kuwa hatari ya vifo kutokana na upasuaji katika nchi zinazoendelea iko juu kuliko walivyotarajia.

Japo njia hiyo ilikuwa ikikusudiwa kusaidia kuokoa maisha ya mama na watoto wao.

Lakini, katika maeneo mengi, hasa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara, sasa inaonekana kuwa hali ni ya hatari zaidi.

Idadi ya wanawake wanaopoteza maisha katika eneo hilo ni mara 100 zaidi ya nchi zilizoendelea kama vile Uingereza.

Na asilimia 10 ya watoto wote hufa wakati au baada ya upasuaji.

Utafiti huo uliochapwa kwenye jarida la masuala ya afya, Lancet, unawataka wanawake katika nchi zinazokabiliwa na changamoto hizo kupata huduma nzuri za upasuaji zenye kutekelezwa na watu wenye utaalamu ili kuhakikisha kuwa upasuaji unafanyika kwa usalama na kitaalamu. **BBC**

# Boeing yashtakiwa kwa ajali ya Ethiopia

**WASHINGTON,** Marekani

KAMPUNI ya kutengeneza ndege ya Boeing imefunguliwa mashtaka nchini Marekani na familia ya mmoja ya abiria waliofariki kwenye ajali ya Shirika la Ndege la Ethiopia mapema mwezi huu.

Watu wote 157 waliokuwa ndani ya ndege hiyo walifariki katika ajali hiyo iliyotokea wakati ndege hiyo ikitokea Addis Ababa kwenda Nairobi.

Ndugu wa Jackson Musoni, ambaye alikuwa ni mfanyakazi wa Umoja wa Mataifa na raia pekee wa Rwanda aliyekuwamo kwenye ajali hiyo, wanadai kuwa ndege sampuli ya Boeing 737 Max 8, zina upungufu wa kiusanifu katika mifumo yake ya kujiendesha.

Ndege zote 371 zinazomilikiwa na mashirika mbalimbali za aina ya 737 Max 8 zimepigwa marufuku kuruka tangu ilipotokea ajali hiyo, ambayo ilikuwa ni ya pili kwa sampuli hiyo ndani ya miezi mitano. Ajali ya kwanza ilitokea Oktoba 2018 nchini Indonesia na kuua watu wote 181 waliokuwamo ndani yake.

**Lakini bado haijajulikana ni lini ndege hizo zaidi ya 300 zilizozuiliwa kusafiri kote duniani mwezi huu zitaruhusiwa kupaa.**

Kampuni ya Boeing bado haijatoa tamko lolote kuhusu kesi hiyo. Wachunguzi pia bado hawajatoa ripoti kamili juu ya sababu hasa ya ajali hiyo kutokea. Jumatano wiki hii kampuni ya Boeing ilitangaza kuwa wamefanyia marekebisho mfumo wa udhibiti (MCA) ambao unahusishwa na ajali zote mbili.

Kama sehemu ya kuboresha ndege hizo, Boeing itaweka mfumo wa onyo kulingana na viwango, ambavyo awali ulikua si wa lazima.

Ndege zilizopata ajali za kampuni ya Lion Air ya Indonesia na Ethiopian Airlines, hazikuwa na mfumo wowote wa kuashiria ajali, ambao lengo lake ni kuwaonya marubani wakati mtambo wa uongozaji wa safari ya ndege unapotoa taarifa kinyume na matarajio.

Boeing ilisema makampuni hayatakuwa yakitozwa pesa za ziada kwa ajili ya kuweka mfumo huo wa usalama wa ndege.

Lakini bado haijajulikana ni lini ndege hizo zaidi ya 300 zilizozuiliwa kusafiri kote duniani mwezi huu zitaruhusiwa kupaa.

Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa Boeing kukubali kuwa kulikuwa na upungufu wa kiufundi kwenye ndege hizo. Awali mamlaka za Marekani zilitetea kampuni hiyo zikidai sampuli 737 Max ni salama.

Shinikizo kubwa la kimataifa dhidi ya ndege hizo lilianza mara tu baada ya ajali ya Ethiopia kutokea. Shirika la Ethiopia lilifuta safari zake zote za ndege aina hiyo mara tu baada ya ajali.

Nchi kadhaa, zikiwamo za Jumuiya ya Ulaya, Canada, China na Rwanda zilipiga marufuku ndege hizo kupaa kwenye anga za mataifa hayo. **BBC**



Muumini akibusu pete ya Papa, ni utaratibu wa Wakatoliki sehemu zote duniani, jambo ambalo hata hivyo anahofia kuwa linaweza kuwa chanzo cha kusambaza maradhi. **PICHA: REUTERS**

# Papa anena kukataza kubusu pete

**VATICAN CITY,** Vatican

PAPA Francis, amevunja ukimya juu ya mkasa wa kuzuia waumini kubusu pete yake, akisema lilikuwa ni suala la kiafya zaidi.

Msemaji wa Vatican Alessandro Gisotti, alisema kuwa Papa alikuwa akihofia kusambaa kwa vijidudu alipokuwa akikutana na waumini wa Kanisa Katoliki siku ya Jumatano.

Wahafidhina ndani ya kanisa walipinga vikali kitendo hicho wakidai Papa anavunja utamaduni wa muda mrefu wa kanisa."Lilikuwa tu ni suala la kiafya," Gisotti alisema Alhamisi iliyopita, akiwaambia wanahabari kuwa yeye mwenyewe alimuuliza Papa juu ya suala hilo.

Gisotti alisema kuwa kulikuwa na watu wengi waliokuwa kwenye msururu wa kumsalimia Papa na yeye akawa na tahadhari juu ya uwezekano wa kusambaza vijidudu.

Kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki mwenye miaka 82 anadaiwa kuwa "hakufurahishwa" na utata huo, msaidizi wa Papa aliliambia shirika la habari la Reuters.

"Papa anapenda kuwakarimu watu na yeye pia hupenda kukarimiwa," alisema Gisotti na kuongeza kuwa Papa hufurahia kuwaruhusu watu kwenye makundi madogo kubusu pete yake.

Mkanda mrefu zaidi wa tukio hilo unaonyesha kuwa Papa aliwaruhusu watu wachache kuinama na kubusu pete yake.

Siku iliyofuata Papa alionekana akiwaruhusu watawa na makasisi kubusu pete yake katika baraza lake kuu la Mji wa Vatican huko Roma.

Pete ya Papa, ya dhahabu inayovaliwa kwenye kidole cha kati cha mkono wa kulia ndiyo alama yenye nguvu zaidi ya utawala wa Papa.


Kubusu pete hiyo ni utamaduni uliasisiwa miongo mingi iliyopita na inachukuliwa kama alama ya heshima na utii kwa kiongozi huyo mkuu wa Kanisa Katoliki. Mara tu baada ya Papa kufariki, pete yake mara moja huteketezwa ikiwa ni kiashiria kuwa utawala wake umefikia kikomo. **BBC**

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watuwengine kujeruhiwa. Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji, mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki cha kusisimua...

# KISANDUKU CHEUSI - **41**

**Na Adam Fungamwango**




"Sikiliza Mapunda, mimi nilikutana na Hellen kwa bahati mbaya na nilimpenda na yeye akanipenda, lakini katika mapenzi yetu alinipa picha ambazo zilikuwa za watu waliofanana, japo mmoja alikuwa amenenepa zaidi kidogo, akaniambia yule ni pacha mwenzake na alifariki kwenye ajali. Tena akaniambia ilikuwa kama ya kupangwa hivi.

Kwa sababu mimi ni askari nilitaka kudadisi, japo alinionya kuwa ni mapema tusubiri siku nyingine. Kwa sababu wewe ulisikia maneno yale, usiku mkaja Tabata Kimanga kumuua nilipoondoka...

Eddy akiwaangalia kwa makini mateka wake.

"Mtu ambaye angenipa urahisi wa kupeleleza alikuwa ni Hellen. Msingemuua tu siku ile angenipa habari yote mapema, saa hizi mngekuwa mmeshapata haki yenu siku nyingi, lakini ilibidi niingie 'chimbo' ili kujua ukweli wote.

Kwanza kabisa ilibidi nipate uhakika kuwa ni kweli Careen alikuwa ndani ya basi la Bomoa Trans. Safari hiyo ilinifikisha Ubungo na kweli nilithibitishiwa kuwa aliondoka siku hiyo.

Nilitaka kujua kama ni kweli alikwenda kwenye maandalizi ya kufunga ndoa au kusalimia. Nilifunga safari ya kwenda Ifakara na kukutana na watu muhimu ambao kwa kiasi kikubwa walinisaidia kwenye upelelezi wangu." Eddy alieleza akiwa kama anawasuta hivi.

"Nassy, binti Sanze mmoja wa abiria, yeye aliniambia kuwa kuna jamaa mmoja mwenye pama ndiyo aliyeomba kushuka kwenda kujisaidia. Na kuona hivyo baadhi ya abiria waliona ni fursa ya kwenda kujisaidia pia.

Cha ajabu yule jamaa aliyeteremka aliacha 'briefcase' yake chini ya kiti cha abiria mmoja, ingawa wengi hawakuona ajabu wala kuhisi kuwa ana nia mbaya. Dakika chache baadaye basi lililipuka na waliokuwa nje kujisaidia ndiyo waliopona.

Waliokuwa kwenye basi walifariki na wengine kupata vilema vya maisha na majeraha ya kudumu. Nassy akaniambia kuwa abiria wote waliopona walikusanywa ili kuwasafirisha makwao. Wakaleta basi. Wote walikuwapo, kasoro yule jamaa mwenye pama. Wao walidhani kuwa kwa sababu alionekana kuwa ni mtu mwenye uwezo, hakuweza kusubiri basi la dezo, akaamua kuendelea mbele na safari yake.

Kwa maelezo hayo mimi nikajua kuwa yule ndiye mlipuaji wa basi hilo. Na kwa bahati nzuri hata wewe mwenyewe umeniambia hivyo tangu juzi ulipokuwa ukinipa mkanda mzima wa mauaji, ukidhani sitopona utaniua.

**Baada ya hapo nikafika hadi kwa wazazi wa Mayambua, wapo kule Ifakara. Mayambua pamoja na kwamba alikuwa akiishi na kufanya kazi Dar, lakini alikuwa ni mwenyeji wa Ifakara na nadhani hiyo ilimfanya kuwa rahisi kumnasa Careen wa Ifakara mwenzake.**

Ungejua kama ulikuwa unamwambia mpelelezi, usingefanya hivyo. Ulijua unamwambia Mayambua. Raia wa kawaida, dhaifu ambaye asingeweza kukufanya lolote lile, au kutoka hai kwenye jengo hili chini ya himaya yako." Eddy alizidi kupasha na kumfanya Mapunda kwa mbali miguu kuanza kumcheza. Kwa hapo tu alipofikia, alianza kuhisi kuwa yupo kwenye matatizo makubwa. Alijua askari yule anajua mengi zaidi na hata yale aliyokuwa akimweleza mwanzo, aliyajua kabla hata hajamwambia.

Mapunda sasa aliamini kuwa yule jamaa ni kweli alikuwa mpelelezi. Tena mpelelezi hasa na si Mayambua kama alivyodhani. Alianza kujuta. Yote aliyoyafanya yalikwenda kama alivyopanga, lakini kosa kubwa alilofanya ni kudhani kuwa askari yule mpelelezi ni Mayambua, mchumba wa mpenzi wake Careen, kiasi cha kutuma kikosi chake kwenda kumteka. Kumbe ilikuwa ni sawa na simba kumtumbukiza kwenye zizi la ng'ombe.

"Nilipotoka hapo nikaenda kwa mama mmoja nadhani unamfahamu. Anaitwa Bi. Mkali. Wewe Mapunda anakufahamu sana. Ni shangazi wa mapacha Hallen na Careen. Yeye alinieleza mengi kuhusu mapacha wake wakivyoachwa yatima bado wadogo, alivyowalea na kuwasomesha hadi walivyokuwa wakubwa.

Alinipa habari zako. Na huko ndipo nilipopata habari zako na kukufahamu. Nilipata jina lako huko na mikasa yote niliyokuwa nahadhithiwa nikaanza kukuhisi.

"Ile barua niliyoifuma kwenye mkoba wa marehemu Hellen ya kumtisha Careen haikuwa na jina la mtu, tena iliandikwa kwa mashine, lakini mkasa alioniambia Bi.Mkali kuwa kuna mtu anaitwa Banson Mapunda alikuwa na uhusiano na binti yake Careen, lakini baadaye ulilegalega na kumpata Mayambua aliyekwenda kutoa barua ya posa upesi kutaka kumuoa.

Kwa maelezo yake nikaunganisha mambo na kugundua kuwa aliyeandika barua ya kumtisha atakuwa ni Mapunda na aliyesababisha ajali atakuwa ni mtu huyo huyo."Eddy alisema huku akitabasamu.

Ilikuwa ni kejeli na kutaka kumuonyesha Mapunda kuwa alichokuwa akikifanya na kuingia gharama kubwa pamoja na kuua watu ili kuficha ukweli, lakini ni kazi bure.

"Baada ya hapo nikafika hadi kwa wazazi wa Mayambua, wapo kule Ifakara. Mayambua pamoja na kwamba alikuwa akiishi na kufanya kazi Dar, lakini alikuwa ni mwenyeji wa Ifakara na nadhani hiyo ilimfanya kuwa rahisi kumnasa Careen wa Ifakara mwenzake.

Huku wakanieleza kila kitu, pamoja na mipango yote. Niliwauliza kama Mayambua aliacha ujumbe, wakaniambia hakucha ujumbe, lakini Mayambua alipojinyonga chini yake walikuta kuna nakala ya CD iliyoonyesha ina nyimbo za mwanamuziki Bob Marley kwa hiyo wakaichukua na kuiweka ndani na wala hawakuwa na wazo lolote lile.

Polisi wa kawaida wao wamekariri kuwa marehemu huacha ujumbe kwenye karatasi, lakini mimi kama mpelelezi mzoefu nilipoambiwa hivyo niliomba nipatiwe hiyo CD.

Nilipoiweka kwenye kompyuta, nilichosikia ni sauti ya Mayambua akieleza sababu za kujinyonga kuwa hawezi kuishi bila Careen. Kwa sababu amekufa na yeye hana sababu ya kuendelea kuishi.

Lakini na yeye kama alivyofanya Hellen alieleza kuwa kifo cha Careen kilipangwa kwa sababu kuna ujumbe alitumiwa unaoonyesha kuwa watu walikuwa wameshamaliza kazi. Pia yeye mwenyewe alikuwa akitishiwa kuuawa na mtu ambaye hamjui, lakini akimtuhumu kumpora mpenzi wake. Kwa mlolongo wote huu nikajua kabisa kuwa hii yote ni kazi ya Mapunda."

Maneno aliyokuwa akiongea Eddy yaliwatisha mpaka mabaunsa wale watatu wa Mapunda.

Tukio alilolifanya mle ndani hadi kuwaweka chini ya ulinzi na jinsi anavyosimulia alivyokuwa akilipeleleza jambo hilo, liliwafanya kuona wamejiingiza kwenye kazi nzito kuliko walivyodhani. Jasho nao lilianza kuwatoka, ingawa walijitahidi kutoonyesha hofu ili kusubiri muda kwani wanaweza kuokolewa na wenzao huko nje iwapo watahisi kuwa wamo hatarini.

"Niporejea Dar, nilitaka kujua kuwa Banson Mapunda ni nani. Na wasaidizi wangu walinileta zaidi ya watu 15 kwenye majina hayo, lakini kulikuwa na jina la mtu huyo linaloonyesha kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji na mmiliki wa Paradiso Hotel.

Ndiyo hoteli ambayo Careen na Hellen walikuwa wakifanyia kazi. Na Mapunda ndiye alikuwa mpenzi wake Careen. Na huyo huyo ndiye aliyeporwa mpenzi aliyeuawa katika mazingira ya kutatanisha.

Nilijua nikija kama mpelelezi nitachukua muda mrefu kupata ninachokitaka. Nikikukamata na kukuhoji tutasumbuana na huwezi kunipa ushahidi wa moja kwa moja. Nilichokifanya ni kujifanya mimi ndiye Mayambua na nikaja ofisi kwako. Nilijua kitu ambacho ukikutana na mtu kama huyo utamfanya. Kwa sababu tayari ulishamtisha.

Kwa bahati mbaya ulijifanya haupo ofisini, niliandika ujumbe na kumpa sekretari wako, nilijua akiupata tu na kuona jina la Mayambua ni lazima ashtuke na kuanza kunifuatilia.

Na kweli ikawa hivyo, hadi wale watu wako waliponiteka. Nilihitaji kutekwa ili kujue haya niliyoyajua kwa wepesi na urahisi zaidi. Ndiyo maana hata wewe mwenyewe ukaniambia kila kitu ulichokifanya juu ya mpango mzima wa kumuua Careen na watu wengine. Hakuna ambacho umekifanya na hakijulikani kwa sasa Mapunda utalipa unyama wote ulioufanya." Eddy alizidi kunguruma.

*Itaendelea Jumamosi*

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 29/03/2019.

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe **12/04/2019** kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka BABATI kuelekea NAMANGA gari hilo lenye namba za usajili: **T827 BCN ,T741 CPB, T985 ABJ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu-mita 17**
   **Upana –mita 3.0**
   **Kimo – mita 3.2**
3. Njia itakayotumika **BABATI hadi NAMANGA kupitia OLDONYOSAMBU** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

xxxxxx

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI


**JOANITHA ELIEZAR RUTAGELEKWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 459 DHL TOYOTA IST. Chassis namba NCP61-0042869. Engine namba 2NZ4017412.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KJN/B.I/VOLIX/4726/19.**

115148102

### KUPOTEA KWA CHETI



**Edgar Emil Kikwilu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0110-0579** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa **mwaka 2013** katika Shule ya Sekondari Ilboru.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**UPR/RB/1319/2019**

115147602

### KUPOTEA KWA CHETI



**Caroline Shayo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S220/326 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1992 kilichotolewa na Tabora Girls Sekondari,

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1896/19**

215148002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MJIBU RUFAA**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**MADAI NAMBARI 05/2019**

**MDAI BANKANIE VICENT**
**Anamdai**

**Mdaiwa No.1. MONICA NDEREKA**
**Mdaiwa No.2. FILBERT NDEREKA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake**
Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMATANO tarehe 10/4/2019 saa 2:30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 27/3/2019.

115147502

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LTD A**NATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 719 CDD.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI**
**MBI/RB/375/2019.**

115147902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MJIBU RUFAA**
**(MCA/84)**
**Mahakama ya wilaya ya Dodoma**
**Madai na. 43/2018**
**Mdai FABIAN EDWARD MESAY**
**MDAIWA Salome John**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 27/03/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa /mmeshindwa kutekeleza Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 21/3/2019

115147802

### CHETI KIMEPOTEA



115147202

**KIBOLA ADAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number: SO 3420556 kilichotolewa na Shaaban Robert Secondary School mwaka 2000.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KW/RB/241/2019.**


## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

## KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga simu: 0767 223 311

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BOATENG KUONDOKA BAYERN MUNICH




**MUNICH,** Ujerumani

BEKI wa Bayern Munich, Jerome Boateng, anapanga kuondoka klabuni hapo kwa kipindi kifupi kijacho, baada ya kusajiliwa kwa Lucas Hernandez kwa euro milioni 80.

Pamoja na Lucas, pia Benjamin Pavard (23) atajiunga na klabu hiyo katika kipindi cha majira ya joto, huku nahodha wa Ajax, Matthijs de Ligt akiwa bado anawindwa.

Bayern tayari ina mabeki wa kati Boateng, Mats Hummels na Niklas Sule, lakini kutokana na umri kuwatupa mkono, miamba hao wa Bavaria sasa wanataka kusajili wachezaji wenye damu changa.

Kwa mujibu wa gazeti la Suddeutsche Zeitung, Boateng ambaye anapanga kuondoka klabuni hapo, bado haijajulikana ni wapi anakwenda.

Hata hivyo, habari zaidi zinasema kwamba klabu za Manchester United, Paris Saint-Germain na Juventus zimeonyesha nia ya kumtaka beki huyo mwenye umri wa miaka 30.

## Inter wamtaka Mourinho au Conte

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter inaangalia uwezekano wa kumchukua ama Jose Mourinho au Antonio Conte ili kuchukua mikoba ya Luciano Spalletti, kama wakiamua kuachana na Muitaliano huyo kwa siku za usoni.

Ushindi wa mabao 3-2 katika 'dabi' dhidi ya Milan kabla ya kupisha mechi za kimataifa ulipunguza machungu ya Nerazzurri, lakini kutolewa kwao kwenye michuano ya Ligi ya Europa na Eintracht Frankfurt kumeonyesha wazi kuwa kuna uwezekano wa kuachana na kocha huyo mapema zaidi.

Gazeti la Corriere dello Sport limeripoti kwamba makocha hao wa zamani wa Chelsea ndio wanaofikiriwa zaidi kuchukua mikoba katika timu hiyo.

Conte amekuwa hana timu tangu alipoondoka Chelsea kipindi cha majira ya joto, lakini ndiye anayeonekana kupewa nafasi kubwa zaidi ya kutua hapo Inter Milan.

Hata hivyo, Mourinho ana historia nzuri zaidi na Inter kwa sababu wakati akiinoa timu hiyo kati ya mwaka 2008 hadi 2010, na alishinda kila kitu, kuanzia Serie A hadi Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2010.

Ingawa bado hajarudi kwenye nafasi ya ukocha tangu alipofukuzwa pale United Desemba mwaka jana.



## Juventus yajitosa kumwania Alderweireld

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeingia kwenye mbio moja za kuwania kumsajiili beki wa Tottenham Hotspur, Toby Alderweireld, huku Manchester United pia nao wakimnyatia.

Alderweireld kwa sasa thamani yake ni pauni milioni 25, kitu ambacho kinaonekana Tottenham wameshindwa kuongeza mkataba na wanaweza kuwa kwenye hatari ya kumwacha akiondoka akiwa mchezaji huru.

Habari za Juventus kumtaka Alderweireld zimekuja baada ya gazeti la The Mirror kudai kwamba mabingwa hao wa Serie A wamemweka kama chaguo lao sahihi kwenye safu ya ulinzi.

Hata hivyo, watakumbana na ushindani kutoka kwa United katika kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. Ingawa wakati wa zama za Jose Mourinho ilionyesha kwamba mchezaji huyo hahitajiki, lakini Solskjaer anaonekana kuvutiwa na beki huyo.

Solskjaer ambaye juzi alipewa mkataba wa kudumu kuifundisha timu hiyo baada ya kuichukua Desemba mwaka jana, ameonyesha wazi kwamba anamhitaji beki huyo kwa ajili ya kuimarisha safu yake ya ulinzi.



HABARI MICHEZO

# Timu ya Taifa Gabon yafutwa

**LIBREVILLE,** Gabon

SERIKALI nchini Gabon kupitia Wizara ya Habari, imetangaza kuifuta rasmi Timu ya Taifa ya Soka, kutokana na kushindwa kufuzu Fainali za Afrika za mwaka huu (AFCON 2019).

Akitoa tamko la kuifuta timu hiyo, Waziri wa Michezo wa Gabon, Alain Claude Billie-By-Nze, amesema kuwa wachezaji wa timu hiyo hawajitumi na wameweka maslahi ya fedha mbele kuliko uzalendo.

"Tunakwenda kuijenga upya timu yetu ya taifa kwa misingi bora, tutawaweka pembeni wachezaji wote waliokosa uzalendo na utaifa na wanaoweka fedha mbele.

"Haiwezekani wachezaji hawajitumi na wanacheza kama wamelazimishwa uwanjani," alisema waziri huyo kupitia televisheni ya taifa.

Mashabiki wengi wa soka wa Gabon wamekuwa wakimshushia lawama mshambuliaji wa timu hiyo ambaye anakipiga katika klabu ya Arsenal, Pierre Aubameyang, kuwa hajitumi uwanjani na amekuwa akijitenga na wachezaji wenzake licha ya mara kadhaa kuisaidia timu hiyo kifedha.

Hata hivyo, Waziri Billie-By-Nze hakufumbia macho tuhuma hizo kwani akizungumza na waandishi wa habari alitupa kijembe kwa kusema, "Watu wanaojiweka mbele kufadhili timu kifedha na hata kiushauri kwa namna nyingine hatuwezi kuwaita tena."

Katika tamko hilo pia ametangaza kuifuta timu ya taifa ya wachezaji walio chini ya miaka 23 na amesema itaundwa upya baadaye, kwa kuwa baadhi ya wachezaji watachukuliwa katika timu ya wakubwa.

Waziri huyo amesema kuwa timu nyingine mpya itatangazwa baada ya siku 60, kuanzia uamuzi huo ulipotangazwa na itakuwa na wachezaji pamoja na kocha mpya ambao wote wataweka uzalendo mbele.

Gabon imeshindwa kufuzu AFCON 2019 kwa kulazimishwa sare ya 1-1 na Burundi kwenye mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi, ambapo Gabon walikuwa wanahitaji ushindi ili kufuzu.





# SOLSKJAER KUWATEMA WACHEZAJI HAWA

**MANCHESTER,** England

BAADA ya Manchester United kumtangaza, Ole Gunnar Solskjaer kuwa kocha wao mpya wa kudumu kwa mkataba wa miaka mitatu, baadhi ya wachezaji wameanza kuingia tumbo joto.

Baadhi ya wachezaji wa United hawawezi kuwa na habari njema kwao na inaweza ikawa ndio mlango wao wa kuondokea.

Wachezaji kama Antonio Valencia, ambaye ni nahodha inawezekana akawa ni mmoja kati ya watu ambao hawajafurahishwa, kwa kuwa hana nafasi kubwa ya kucheza kuelekea mwisho wa msimu. Pia Alex Sanchez pamoja na kuwa aliamini anaweza akarudi vizuri uwanjani, lakini inaelezwa Solskjaer hafikirii hivyo na sasa ameonyesha nia ya kuwataka wachezaji Jadon Sancho na Callum Hudson-Odoi, huku hatima ya Sanchez inaweza kuwa ndogo zaidi kwa siku zijazo.

Fred ambaye alisajiliwa kwa dau la pauni milioni 52 na Matteo Darmian hawa kuna dalili nyingi kuwa hawatakuwa na nafasi kubwa ya kucheza chini ya Solskjaer, hivyo inadaiwa hawezi kuendelea kuweka rehani nafasi zao.

Marcos Rojo kwa mujibu wa sera za usajili wa wachezaji wa kigeni wa United, huyu aliongezewa mkataba mwaka uliopita, lakini amekumbana na wakati mgumu kiasi cha kuanza mechi nne tu tena sio chini ya utawala wa Solskjaer, hivyo inawezekana akaondoka.

# *Leicester City kumkumbuka mmiliki wao leo*

**LONDON,** England

KLABU ya Leicester City, leo Jumamosi, itasherehekea kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa ya mmiliki wa klabu hiyo marehemu, Vichai Srivaddhanaprabha.

Uongozi wa Leicester City ili kumkumbuka na kumuenzi Srivaddhanaprabha umepanga kuwa leo hii itakuwa siku maalum.

Leicester Jumamosi hii itakuwa kwenye Uwanja wa King Power kucheza dhidi ya AFC Bournemouth.

Hivyo ili kusherehekea kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa ya Srivaddhanaprabha, kila shabiki atakayekuwa anaingia uwanjani atapewa bia au maji na cupcake.

Mmiliki na mwenyekiti wa timu hiyo marehemu, Srivaddhanaprabha alifariki Oktoba 29, mwaka 2018, akiwa katika helikopta yake binafsi iliyoanguka dakika chache baada ya kupaa kutokea kwenye Uwanja wa King Power.

Mmiliki huyo alikuwa anatoka kuangalia mchezo wa Leicester City dhidi ya West Ham United iliyomalizika kwa sare ya 1-1.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAKARIBIA KUMSAJILI RABIOT

### Ni katika mchakato wa kuziba pengo litakaloachwa na Modric katika kikosi...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imetajwa kuanza mchakato wa kumsajili kiungo wa Paris St-Germain, Adrien Rabiot, ambaye amekosa namba katika kikosi hicho cha vigogo wa Ufaransa, gazeti la The Mirror limeandika.

**Taarifa zilizopatikana zinaeleza kuwa tayari makubaliano yameshafikiwa kati ya Rabiot na mabingwa hao wa Ulaya.**

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23 hajacheza mechi hata moja ya vinara hao wa Ligue 1 tangu Desemba mwaka jana baada ya kukataa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Mfaransa huyo, ambaye atakuwa mchezaji huru katika majira ya kiangazi, pia amesimamishwa na klabu hiyo baada ya kufanya utovu wa nidhamu wakati timu yao ikifungwa na Manchester United kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia inaelezwa kuwa Liverpool na Arsenal pia wameonyesha nia ya kumwihitaji Rabiot, ambaye aliwahi kufanya kazi na kocha wa Gunners, Unai Emery, ilipokuwa akiifundisha timu hiyo ya makao makuu ya Ufaransa.

Barcelona na Rabiot tayari wameshasaini mkataba wa awali, lakini klabu pamoja na mchezaji huyo bado hawajafikia makubaliano katika malipo binafsi.

Mchakato wa usajili huo ni moja ya nafasi zilizoanza kuonekana ndani ya kikosi hicho cha Real Madrid baada ya kumrejesha klabuni hapo, Zinedine Zidane.

Zidane alikuwa pia na mipango ya kumsajili kiungo huyo katika majira ya joto mwaka jana kabla ya kufikia uamuzi wa kuondoka klabuni hapo, licha ya kuwa ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Timu hiyo maarufu kwa jina la Los Blancos pia inatajwa kuwa kwenye mchakato wa muda mrefu wa kusaka mrithi wa Luka Modric, huku Paul Pogba naye akitajwa kutakiwa na vigogo hao.

Hata hivyo, Rabiot ambaye atakuwa mchezaji huru atakuwa katika nafasi nzuri na gharama nafuu ukilinganisha na mpinzani wake.

## ZISIKUPITE

### POGBA MTEGONI MADRID

REAL Madrid inajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 125 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Manchester United Mfaransa, Paul Pogba (26). ***(Sun)***

### ZIDANE AJAZWA MANOTI

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amepewa kiasi cha pauni milioni 430 kwa ajili ya kufanya usajili katika kipindi cha usajili cha majira ya joto na tayari klabu hiyo imeweka wazi nia ya kumtaka straika, Kylian Mbappe (20) wa Paris St-Germain na mshambuliaji Mbelgiji, Eden Hazard (28) kutoka Chelsea. ***(L'Equipe, via AS)***

### HUDSON-ODOI KUONGEZWA DAU

CHELSEA inataka kumpa mkataba mpya nyota wake, Callum Hudson-Odoi (18), ambao utamfanya awe analipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki ili akubali kubakia hapo Stamford Bridge. ***(London Evening Standard)***

### HENRY KUREJEA UBELGIJI

STRAIKA wa zamani wa Ufaransa na Arsenal, Thierry Henry, ambaye Januari mwaka huu, alifukuzwa na Monaco baada ya kudumu nayo kwa miezi mitatu, anatarajia kurejea Ubelgiji kumsaidia kocha mkuu wa timu hiyo, Roberto Martinez. ***(Mirror)***

### JIMENEZ KUTUA WOLVES

WOLVES inajiandaa kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Mexico, Raul Jimenez (27), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Benfica kwa dau la pauni milioni 25 ambalo litaweka rekodi katika timu hiyo. ***(Telegraph)***

### BENITEZ ATAKIWA CHINA

KOCHA wa Newcastle United, Rafael Benitez, ambaye anatarajia kumaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu, anatajwa kuwaniwa na Guangzhou Evergrande kama kocha wa sasa, Fabio Cannavaro ataondoka na kuchukua mikoba ya kuifundisha Timu ya Taifa ya China. ***(Mirror)***

### KOULIABLY NJIA PANDA

KOCHA Carlo Ancelotti anasisitiza kuwa Napoli haitalazimishwa kumuuza beki wake mwenye thamani ya pauni milioni 130, Kalidou Kouliably (27), ambaye amekuwa akiwindwa kwa muda mrefu na Manchester United.***(Mail)***

### SOLSKJAER AFUNGUKA

OLE Gunnar Solskjaer ameweka wazi kuwa mawakala mbalimbali walikuwa wanawasiliana na Manchester United kwa ajili ya kujaribu kuwanunua wachezaji wa timu hiyo katika kipindi cha majira ya joto. ***(Sky Sports)***

### SANCHO, VARANE SOKONI

NYOTA wa Dortmund, Jadon Sancho (19) na Rafael Varane (25) wa Real Madrid wanatajwa kuwa ndio wachezaji muhimu wanaotakiwa kutua Man United. ***(Independent)***

### ALDERWEIRELD KITAELEWEKA

JUVENTUS inajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 25 kilichotajwa katika mkataba wa beki wa Tottenham, Toby Alderweireld (30), wiki mbili kabla ya dirisha la usajili wa majira ya joto kufunguliwa. ***(Mirror)***

### BAYERN YAAHIDI KUJIPANGA

VIGOGO wa Ujerumani, Bayern Munich, wanajipanga kuwekeza katika kiwango cha juu katika kipindi cha usajili cha majira ya joto. ***(Marca)***

# KIKAPU, RIADHA WATAMBA KUFANYA VIZURI OLIMPIKI

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

TIMU ya Taifa ya kikapu na riadha zimeaswa kupambana ili kufanya vema katika mashindano ya Afrika ya Kamati za Olimpiki (Anoca) Kanda ya Tano yaliyopangwa kufanyika kuanzia Aprili 2 hadi 6 mwaka huu, jijini Kigali, Rwanda.

Timu hizo zinatarajia kuondoka nchini kesho na tayari zimeagwa na kukabidhiwa bendera ya taifa na Mkuu wa Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, Assumpter Mshama, katika hafla iliyofanyika jana kwenye Ukumbi wa Filbert Bayi.

**Mshama alisema kuwa anaamini timu hizo zimefanya maandalizi mazuri na zinakwenda kupambana katika mashindano hayo na hatimaye kurejea na ushindi.**

"Sitegemei mtaiangusha nchi, mmenihakikishia mtafanya vizuri na Watanzania wanawaombea hivyo, mtakaporejea na medali nitakuja uwanja wa ndege kuwapokea," alisema kiongozi huyo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Daud Maiga, alisema wanahitaji kuweka rekodi ya kuwa mabingwa katika mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya kwanza.

"Tumejiandaa kwa ushindani, niwahakikishie tu Watanzania kwamba wajiandae kutupokea na medali, tumejiandaa kikamilifu na tuna uhakika wa kurudi na ushindi," alisema Maiga.

Katibu Mkuu wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Filbert Bayi, alisema timu itaondoka Jumapili saa 10 jioni na ndege ya Shirika la Rwanda.

Alisema katika mashindano hayo, Tanzania itawakilishwa na wanariadha wanne na kocha wao atakuwa Mwinga Mwanjala, huku akiongeza kuwa timu ya kikapu inaundwa na nyota wanne.




Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasitha Mboneko, fimbo nyeupe kwa ajili ya kutembelea watoto wenye ulemavu wanaosoma katika Shule ya Msingi Buhangija, ambayo imepata msaada wa vifaa vya kuwasaidia kuona, kusikia na michezo. Benki ya NMB imetoa misaada kwa shule nne mkoani Shinyanga, ambapo kila moja ilipata vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni tano. **NA MPIGAPICHA WETU**

## SportPesa yajikita Racing Point Bahrain

**SAKHIR,** Bahrain

MSIMU mpya wa Formula One kwa mwaka 2019 umeendelea kutikisa vilivyo, huku bila shaka kwa wale wapenzi wa mbio za magari maarufu kama langa langa watakuwa wanaendelea kupata burudani ya aina yake.

Tayari mbio za Melbourne zilizofanyika nchini Australia zimemalizika kwa dereva, Valtteri Bottas (pichani) kutoka timu ya Marcedes kuibuka kinara kati ya madereva 20 walioshiriki mbio hizo kwa kujikusanyia pointi 26.

Katika mbio hizo zilifanyika Machi 14 hadi 17, madereva Lance Stroll na Sergio Perez waliiwakilisha timu ya Racing Point inayodhaminiwa na kampuni ya michezo ya kubashiri ya SportPesa.

Stroll kwa upande wake alimaliza katika nafasi ya tisa akijikusanyia pointi mbili, huku Perez akimaliza katika nafasi ya 13.

**KUELEKEA BAHRAIN**

Baada ya mzunguko wa Melbourne kumalizika, hatimaye patashika ikahamia nchini Bahrain ambapo hapo jana madereva 20 walitimua vumbi wakiwamo Stroll na Perez kutoka timu ya SportPesa Racing Point.

Lance Stroll raia wa Canada ana matarajio makubwa kuelekea mbio hizo za Bahrain, huku akizungumzia mbio zilizopita za Melbourne.

"Nafikiri Bahrain ni moja ya sehemu za kisasa kwa Formula One. Kuna mizunguko mizuri yenye kona za kiufundi. Huwa tunaburudika pindi tunapokuwa Bahrain.

"Lilikuwa ni jambo zuri kupata pointi kwenye mbio za kwanza (Melbourne). Ilikuwa ni moja ya zile siku ambazo tulipigana juu chini kuanzia mwanzo hadi mwisho na hakika mbinu zetu zilifanya kazi," alisema Stroll.

Naye Meneja wa SportPesa Racing Point, Otmar Szafnauer, alisema kuwa wamejifunza kwenye mbio zilizopita na wanategemea kufanya maboresho makubwa kuelekea mbio hizo za Bahrain. Mbio hizo za Bahrain zilizoanza rasmi jana, na zitamalizika leo, huku mbio zinazofuata zitafanyika China kuanzia Aprili 12 hadi 14 mwaka huu.






**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2. Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3. Simba | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4. Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5. Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6. Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7. TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8. Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9. Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10. Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11. Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12. Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13. JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14. Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15. Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16. Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17. Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18. Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19. Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20. African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

Michezo
Jumamosi Machi 30, 2019
Nipashe



Madrid yakaribia kumsajili Rabiot

UKURASA 30




Wachezaji wa Lipuli FC wakishangilia baada ya kufunga bao la kwanza katika mechi ya hatua ya robo fainali dhidi ya Singida United iliyochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa CCM, Samora Iringa. Lipuli ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MAKTABA**

# Yanga yaipania Alliance FA Cup

## ●●● Yasema umakini ndio utawasaidia wakati Azam FC ikitangulia nusu fainali...

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, amesema kikosi chake kina kila sababu ya kuibuka na ushindi katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Alliance FC utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini hapa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mwandila alisema mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani na wamejipanga kucheza kwa umakini zaidi kutokana na wapinzani wao kujiandaa vema.**

Mwandila alisema kuwa Alliance FC sio timu ya kubeza na kwa sababu hiyo anatarajia kupanga kikosi imara ambacho kitaingia kwa kazi moja ya kupata ushindi.

"Nashukuru tupo vizuri, mazoezi ya jana (juzi) yametupa picha kamili kuelekea mchezo wa kesho (leo)... tutacheza kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wetu," alisema Mzambia huyo.

"Huu mchezo ni muhimu sana kwetu, tunafahamu kuwa ushindi utatusogeza mbele zaidi kuelekea kwenye ndoto yetu ya kuchukua ubingwa wa mashindano haya," alisema Mwandila.

Aliongeza kuwa kurejea kwa kiungo, Thaban Kamusoko, kumeongeza hamasa katika kikosi chake ambacho leo kitamkosa nahodha wake, Ibrahim Ajib ambaye ni majeruhi. Naye Kocha Msaidizi wa Alliance FC, Kessy Mziray, alisema kuwa wako tayari kwa mchezo huo, lakini wanaihofia zaidi safu ya ushambuliaji ya Yanga ambao ina wachezaji wenye uzoefu na mashindano mbalimbali.

"Tumeelekeza nguvu zaidi katika safu ya ulinzi, tunafahamu Yanga ni nzuri na wana safu nzuri ya ushambuliaji, hivyo ni lazima mabeki wetu wawe makini kuwadhibiti. Hatupo tayari kuona tunapoteza tena mchezo mbele ya Yanga..., tutacheza kwa tahadhari, na pia tunapaswa kuwa makini muda wote wa mchezo," alisema Mziray.

Kikosi cha Yanga kilitua jijini hapa juzi na kufanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Chuo cha Ualimu Butimba kabla ya jana jioni kuhamia kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Katika kujiandaa na mchezo huo, huku wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Alliance ilikwenda kuweka kambi yake ya muda nchini Rwanda.

Mshindi wa mechi ya leo atakutana na Lipuli ya Iringa katika mchezo wa hatua ya nusu fainali.

Wakati huo huo, Azam FC imefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali baada ya kuifunga Kagera Sugar bao 1-0 katika mchezo uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Joseph Mahundi katika dakika ya 79, sasa Azam itakutana na KMC katika hatua hiyo.

# Simba yapeleka shangwe Morogoro

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba imetua salama mkoani Morogoro, huku meneja wake, Patrick Rweyemamu, akisema kuwa wamekwenda kwa kazi moja ya kusaka pointi tatu.

Simba inayonolewa na Mbelgiji, Patrick Aussems, inatarajia kuikaribisha Mbao FC kutoka jijini Mwanza katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Rweyemamu alisema kuwa wamejiandaa vema kuelekea mchezo huo na wamejipanga kumaliza "uteja" dhidi ya Mbao FC ambayo imekuwa ikiwasumbua katika mechi za mashindano mbalimbali wanapokutana.

"Tumefanya maandalizi mazuri kuelekea mtanange wetu na Mbao, wachezaji wote wako kamili, hakuna matatizo yoyote mpaka muda huu, tunategemea kufanya mazoezi huko Morogoro, tunawaheshimu Mbao, katika msimu uliopita walitupa changamoto, na msimu huu katika mechi ya kwanza hatukufanya vizuri," alisema Rweyemamu.

Alimtaja kipa chaguo namba moja wa timu hiyo, Aishi Manula kuwa naye amesafiri na kikosi hicho baada ya afya yake kuimarika tofauti na ilivyokuwa inadaiwa kwamba anaweza kukosekana katika mchezo huo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >